

SHAABAN ROBERT

WASIFU WA SITI BINTI SAAD


SHAABAN ROBERT
WASIFU WA SITI BINTI SAAD

WASIFU WA SITI BINTI SAAD

SHAABAN ROBERT

YALIYOMO

Utangulizi

Maisha ya utoto kijijini

Mashaka yaliyoshindwa mjini

Kufaulu kwake tarabuni

Pingamizi na wivu

Jawabu ambalo halikutazamiwa

Mabadiliko ya heri

Safari na kuenea kwa sauti yake

Tabia njema

Kijikimu kistahiki

Orodha ya maana ya maneno

Bwana mtawala

UTANGULIZI

Mkutano wangu wa kwanza na Siti Mwimbaji ulikuwa si miaka mingi iliyopita. Ulikuwa katika Februari, 1950, nilipozuru Unguja kwa muda wa juma moja. Katika mambo yangu mengine nilipokwenda kule, nilikuwa na haja ya kuonana na mwimbaji huyu ambaye sifa zake nilikuwa nimezisikia kwa muda mrefu.

Nilitafuta mtu aliyezoeana naye kunipeleka nyumbani kwake akanijulishe. Ilikuwa saa nane asubuhi nilipofika nyumbani kwake siku ile. Nilipobisha hodi mlangoni, mtu mmoja alitokea akasema kwamba Siti alikuwa kitandani bado kwa sababu alikuwa mgonjwa.

Habari ile haikunipa tamaa ya kumwona. Nilianza kushuku kwamba ilikuwa ndege mbaya kwangu. Walakini, kwa bahati njema, mara ile ile mtu mwingine alitoka ndani akasema kama

niliweza kumngoja pale kwa muda wa dakika chache ningalionana naye. Basi nilingoja. Baada ya robo saa nilikaribishwa ukumbini nikaketi kitini.

Punde baadaye, mwanamke wa kimo cha wastani na unene wa kadiri alitoka chumbani akanena kwamba yeye alikuwa ndiye Siti, Nilisimama nikaamkiana naye vizuri kwa kushikana mikono, kisha tukakaa vitini kwa kuelekeana.

Nywele nyeusi kichwani mwake zilionekana na miali michache sana ya mvi, ingawa alikuwa mtu mzima wa kutosha kuwa nyanya. Alipoita paka wake, Kiote na Chanjia, sauti yake ilikuwa imara sana.

Nini, uzee ulianza katika miaka ya arobaini! Ilikuwa dhihaka tupu. Kama ungalipata kumwona mwanamke huyu katika umri wake wa miaka sabini, ungeliweza kuamini kwamba uzee ulianza baada ya miaka sabini.

Kwa kuwa nilihadharishwa kuwa alikuwa mgonjwa, chemchemi yangu ya maswali haikupata nafasi ya kuchemka kama ilivyozoea. Nilichelea

kumchosha nikamngoja aanze kusema, Alianza.

Alisema kwamba falau asingalikuwaa mzembe katika matumizi yake, angaliweza kukusanya fedha nyingi baada ya kujinunulia nyumba na vitu vingine kadha wa kadha kwa kuimba.

Nilipomwomba kama aliweza kunifadhili kwa picha yake akakubali kwenda nami kwa mpiga picha. Alasiri ya siku ile ile tulikwenda kwa mpiga picha tukapiga picha yake. Sikufikiri kwamba ile ilikuwa mara yangu ya kwanza na ya mwisho kuonana naye, wala kwamba picha ile niliyokuwa nayo mikononi mwangu ilikuwa kama ukumbusho wake wa mwisho.

Nilirudi Tanganyika nimekata shauri ya kudhuru tena Unguja

kwa kusudi la kutafiti tena Habari zake nipate kuandika wasifu wake, lakini baada ya miezi minne - miezi minne tu - mauti yake yalitangazwa. Alifariki dunia katika Juni, 1950. Ulikuwa msiba mkubwa Unguja na Afrika Mashariki nzima.

Mimi, ambaye nilitamani kuandika wasifu wake sikujua pahali pa kuanzia wala pa kukomea, nilikuwa kama mwanamaji ambaye alipeperushwa katika mashua isiyo sukani katika usiku wa Dhoruba. Hatari yake ya kumezwa na mawimbi makali kila kipindi ilikuwa kama hofu yangu ya kutumbukia wakati wowote katika makosa makubwa.

Nilipokuwa katika hofu hii, nilijiona vilevile katika deni kubwa la kulipa. Lilikuwa si deni la fedha. Sikudaiwa na mtu yeyote. Nilikuwa katika deni ambalo sikuahidi kwa mtu, lakini niliyo jiahidi mimi mwenyewe kutimiza. Sikuweza kutoka ndani yake. Nilikuwa katika wajibu wa kiungwana. Kazi ya kutimiza wajibu huu ilikuwa ngumu, lakini nimejaribu kuifanya.

Shaaban Robert,

Tanga,

Tanganyika Territory.

Alikuwa ni kinanda

Afrika Mashariki

Na watu wakampenda

Kwa haw ana kwa ashiki

Ndipo bidi ikaenda

Kutunga kitabu hiki.

MAISHA YA UTOTO KIJIJJINI

Nchi hazikuhesabu ubora wa Watoto wake, mpaka Watoto wale walipokuwa wamepita Maisha ya mwili, roho zao zilipokuwa zimevuka ng'ambo ya pili ambako upeo wa macho haukuweza kufika wala mwito wa mwanadamu haukuweza kusikilika, tena baada ya miili yao ilipokuwa imekwisha changanyika na vumbi la ardhi, na thamani yao yote kama viumbe bora ilipokuwa imepotea.

Kwa manzili kama haya mashaka makubwa ya kupata Habari zao yametokea mara kwa mara, kwa sababu alama imara za nyayo zao zilikuwa zimekwisha futika mahali walipokanyaga, matendo yao mema yalikuwa yamezibwa na giza, maneno yao ya maana na mvuto yalikuwa yametoweka masikiani mwa watu wazima ambao fikira zao zilikuwa zimetatizika.

Rai ya kuzuia hasara kama hii haijapatikana bado, kwa sababu dunia imezoea sana kuwa pofu ya kuona bidii na matendo mazuri ya Watoto wake katika wakati wa Maisha yao ya mwili. Katika giza la sahau kuu ndipo ilipozinduka katika usingizi wake mzito, ikajaribu kuokota na kuunga pamoja viungo vya mkufu wa Maisha bora, yaliyofumka kwa mapigo makali na mazito yaliyoangukia Watoto wake walipokuwa wakijipambanua.

Miongoni mwa majina mashuhuri ya watu wa Afrika Mashariki pametokea jina la mwanamke mmoja. Mwanamke mwenyewe aliitwa Siti binti Saad. Siti alikuwa binti wa wazazi Waafrika wa makabila mawili mbalimbali. Kuumeni alikuwa Mnyamwezi na kukeni alikuwa Mzigua. Wazazi wake wote wawili walikuwa wazaliwa wa kisiwa cha Unguja.

Alikuwa mwanamke wa majina mawili katika nyakati mbalimbali. Kwa muda wa miaka thalathini na moja ya kwanza alijulikana kwa jina la Mtumwa binti Saad, na katika miaka thelathini na tisa mingine alikwenda kwa jina la Siti binti Saad.

Mwanamke huyu alizaliwa Fumba na wazazi waliokuwa maskini. Baba yake alikuwa mkulima na mama yake alikuwa mfinyanzi. Katika uzazi

wake alifuatwa na ndugu wanaume wawili, Musa na Mbaruku, na umbu mmoja aliyeitwa masika. Fumba kilikuwa Kijiji kimoja katika vijiji vya Kisiwa cha Unguja. Kadiri ya umbali wa maili kumi na nne ulikuwa kati ya Mji wa Unguja na Fumba.

Tarehe, siku na wakati hasa wa uzazi wake vilikuwa vitu visivyojulikana. Wazazi wake walikuwa maskini na wajinga wa kusoma, hawakushughulika na kuweka shajara la vitu vidogo kama wakati, siku au tarehe ya uzazi wa mtoto wao. Walakini, kwa kukisia ilidhaniwa kwamba tukio la uzazi wake lilitokea katika mwaka wa 1278 A.H au 1880 A.D., katika wakati, siku na tarehe ambayo haikujulikana.

Kama wazazi wake walivyokuwa, Siti hakupata kuona maisha ya chuo chochote katika utoto wake. Fauka ya hilo, kitabu kilikuwa kama fumbo ngumu sana hata katika utu uzima wake, alipokuwa amezungukwa na ufahari.

Watu walioonana na Siti katika utoto, wake hawakudhani hata mara moja kwamba maumbile yalikuwa yamekusudia kumtoa katika giza la sahau, na kumtia katika nuru ya umaarufu baadaye.

Kadhalika, ilikuwa si watu wale tu, lakini hata baba na mama yake walikuwa hawajui kabisa kwamba maumbile yalikuwa yamemwekea binti yao akiba ya umaarufu mkubwa katika wakati

ujao.

Akiba za wanadamu zilizokuwa katika ghala ya maumbile yao zilitatiza hata watabiri hodari kuzitabiri kwa usahihi wowote. Pazia zito lilining'inia daima daima mbele yao. Macho yao hayakuweza kalipenya hata walipokuwa karibu nalo.

Labda macho machache yaliyodhaniwa wakati wa utoto wake yalikuwa kwamba alicheza vizuri na Watoto wenzie. Labda usichana wake alikuwa mcheshi tena mvivu kidogo. Yamkini ufinyanzi wake wa kwanza haukutoa vyungu vizuri. Alionekana kama msaidizi katika maskani madogo ya wazazi wake maskini. Utajiri wowote alioweza kuwaletea ulikuwa mahari ya makumi machache ya shilingi wakati wa arusi yake.

Mwanzo na mwisho wa mawazo ya mtu wa Fumba juu ya Siti ulikuwa kama huo. Palikuwa hapana mtu hata mmoja aliyevuka mpaka wa mawazo hayo akatazamia kwamba tukio jingine lolote liliweza kutokea kwa msichana huyu. Bahati yake ya wakati ujao ilikuwa katika siri kwa watu wote wa kwao.

Kama Kijiji cha Siti kilishindwa kuona dalili yoyote iliyotabiri umaarufu wake katika wakati wa utoto wake, kinyume chake kilikuwa kwamba yeye aliweza, kama kwamba kwa uchawi, kuacha alama isiyofutika ya umaarufu katika kijiji hiki kwa kutia jina lake katika shajara ka ukumbusho wa Fahari kubwa..

Siti alikuwa akienda mjini pamoja na wenzie. Vyungu alivyofinyanga yeye mwenyewe alivichukua juu ya utosi wa kichwa chake akaviuza. Kwa uchukuzi kama ule hapana shaka kwamba wakati mwingine, alipoteleza au alipokwaa mguu, vyungu vyake viliponyoka kichwani vikaanguka chini magae matupu. Hapo ilimpasa kurudi kwao na machozi usoni badala ya fedha mkononi..

Ingawa vyungu vilipendwa sana na wapishi wa zamani zile kama sufuria zilivyo sasa, lakini hvikuleta pato kubwa kwa mfinyanzi. Ilikuwa kazi ya kijungujiko tu.

Nguo alizozoea kuvaa zilikuwa kaniki mbili tu. Alijifunga kaniki moja kifuani akajitanda ile ya pili mabegani. Katika mavazi haya hafifu alikwenda akarudi maili ishirini na nane kati ya Fumba na Unguja.

Alizunguka vichochoro visivyohesabika katika Mji wa Unguja akitafuta huku na huko wanunuzi wa vyungu vyake katika kila mlango wa nyumba.

Katika kila hatua moja njiani alinadi kwa sauti kuu, Vyungu, vyungu, vyungu vizuri, nunueni! Vyungu kwa bei rahisi

Jasho lilimiminika kama maji mwilini mwake kwa mzigo mzito uliokuwa juu ya kichwa chake. Baadhi ya watu walinunua vyungu vyake, wengine wakambeza tu. Alikuwa hana viatu vya kuvaa miguuni. Alikwenda miguu mitupu kabisa katika Kiangazi au Masika, Msimu au Kipupwe, katika miaka yote aliyofanya kazi hii.

Yamkini alipokuwa akinadi vyungu vyake kwa sauti kuu mjini, mtu fulani alinong'ona akasikiwa na Siti kwamba sauti yake ilikuwa nzuri kwa kutumbuiza watu badala ya kunadi vyungu. Kama ndivyo ilivyokuwa, ilikuwa si ishara mbaya kwa msichana huyu katika wakati wake ujao. Au pengine, wakati alipokuwa akizunguka huku na huko mjini, hewa ya Maisha mapya ya mjini ilitambaa polepole moyoni mwake.

Ubaya wa sura ya Siti hukutajwa wakati ule kwa sababu kule kijijini alikuwa hana mwivu. Ufinyanzi ulikuwa kama kazi nyingine za desturi kwa watu wote. Haukupoteza mawazo ya watu katika uadui wala wivu wa kutisha kama mambo mengine yalivyokuwa katika dunia.

Hata kama Siti alikuwa hana sudusu ya uzuri wa Zuhura, lakini hilo halikuwa pingamizi ya furaha ya arusi kumjia. Kama wanawake wengine, aliposwa kwa shauku ya mapenzi mengi sana akaolewa na Rajabu, mume aliyekuwa kufu yake.

Ajabu kubwa iliyokabili watu mara kwa mara katika Maisha yao ilikuwa kwamba bwana arusi mzuri na bibi arusi mzuri aghalabu hawakukutana, kadhalika bibi harusi mzuri aghalabu hawakukutana, kadhalika bibi arusi mbaya na bwana harusi mbaya walikuwa kwa nadra. Wanaume wengi sana wabaya walioa wanawake wazuri, na wanawake wengi wazuri waliolewa na wanaume wabaya. Watu walijibadili kama sarafu katika ndoa.

Sura maalumu ilikuwa si kinywaji cha kuzima kiu kali ya mapenzi. Mapenzi yalitii Zaidi amri ya shauku kuliko yalivyotii ushawishi wa sura.

Matokeo ya ndoa ya Siti na Rajabu yalikuwa binti mmoja aliyeitwa Mariyam. Mariyam na mama yake walikuwa kama shilingi kwa ya pili.

Zaidi ya kuwa mfinyanzi, mke na mama wa Watoto. Siti alikuwa na fikira nyingine sasa. Ususi na ushoni wa mikeka yalikuwa mambo madogo kwake. Alitaka mabadiliko na matendo mapya. Alichoka kushikilia mambo ya zamani yaliyokuwa katika Kijiji chake. Hakutaka kukaa katika duara ndogo ya mila ngumu iliyozuia ushirika wa mwanamke.

Alikuwa kijana bado. Afya yake ilikuwa kamili, na mwili wake ulikuwa juu ya uchovu wa kila namna. Majivuno ya uhai yalimshawishi katika

ujasiri wa kutembea katika ulimwengu wa

ajabu. Kwa ujasiri huu alionyesha waziwazi kwamba mila ile ngumu ililazimu kuhidiwa au kutanguliwa kabisa. Wanawake waliweza kushiriki vema katika mambo mengi ya Maisha.

Kama mapenzi ya Siti ya Kijiji chake yalikuwa makubwa, mapenzi ya ujasiri wake katika Maisha mapya yalikuwa si madogo vilevile. Alikuwa hana starehe kwa sababu mambo mawili haya yalikuwa yakipingana katika moyo wake wakati wote. Alikuwa hana mshauri wa kushiriki wa kushiriki naye siri kama ile.

Aliwaza, akaota, aliota, akawaza mchana na usiku kwa muda mrefu jambo gani lilipasa kuchaguliwa. Mwisho, kwa sikitiko kubwa moyoni mwake, alilazimu kuhama Fumba, Kijiji kilichoona uzazi wake.

Alikusudia kuhamia wapi?

Mjini, kama aliweza kupata pahali pakukaa.

Kule ambako wakati alipokuwa akiuza vyungu vyake, aliona baadhi ya watu ambao alidhani kwamba aliweza kushindana nao, kama aliweza kupata nafasi kati yao ya kujaribu bahati yake ya wakati ujao. Siti alikuwa ratibu hodari wa mambo yake mwenyewe, akakutana na nafaka kubwa sana kuliko ilivyotokea kwa msichana mwingine yeyote wa Fumba wakati ule. Aliondoka kwao bila kitu kingine isipokuwa kaniki mbili zilizokuwa juu ya Ngozi yake.

MASHAKA YALIYOSHINDWA MJINI

Siti aliyapa kisogo maskani yake madogo ya Fumba akashika njia ya mjini. Alipofika Mtoni, Kijiji kingine cha Kisiwa cha Unguja, alivunja safari yake. Toka pale hata mjini ulikuwa mwendo wa maili nne, ilikuwa katika Rajabu 1308A.H au Februari 1910A.D. Katika Kijiji hiki alikaa kwa Ali Saudi. Katika mwaka wa 1309A.H au 1911A.D aliondoka Mtoni pamoja na Musa Bulushi akaenda Unguja.

Hapa mjini alipumua hewa mpya. Ilikuwa ni safi kama ile ya shamba, lakini ilikuwa sulu nzuri ya kukwatua jina lake. Alijaa tamaa kwamba nyota yake iliyokuwa katika mawingu itang'aa siku moja. Na kwa hakika hili lilitimia.

Maisha yake katika mji yalichanganyika sana na yale ya mtu mmoja aliyeitwa Muhsin Ali. Mtu huyu alikuwa mpiga udi mahiri, naye ndiye aliyemfundisha Siti kiarabu na kuimba. Mwalimu wa ajabu na mwanafunzi wa ajabu walikutana katikati ya mji. Laiti Siti asingalikutana na mtu huyu, hadithi yake ingalikuwa vingine kabisa. Labda isingalistahili taabu ya kuisimulia ulimwenguni.

Siti alikuwa na kipawa cha sauti, lakini alikuwa hajui jinsi ya kukikuza wala kukipalilia. Hakujua vilevile jinsi ya kushika pahali pake katika tamasha. Alikuwa hana msingi wowote wa kujenga kuta za ustawi wake. Alikuwa mwanagenzi tu aliyetoka kijijini, katika Maisha ya amani, akajitia mjini, katika Maisha ya ghasia.

Kazi yoyote bila kunga Fulani ilikuwa haiwezekani. Kama Siti hakuona hili kwanza, aliliona waziwazi sasa. Ilikuwa kweli tupu, akashukuru bahati ya kukutana na urafiki wa Muhsin.

Urafiki kati ya Siti na Muhsin

ilikuwa bahati njema sana kwa wote wawili. Bahati yenyewe ilidumisha ari ya mwalimu duniani wakati mifupa yake ilipokuwa baridi kaburini,

ikampeleka mwanafunzi katika heri kubwa. Wote wawili wamefariki dunia. Muhsin alitangulia, Siti alifuata.

Kwa urafiki huo jiwe la kwanza la msingi wa fanaka ya Siti liliwekwa. Siti alijifundisha kwa bidi kubwa. Imesemwa kwamba fahamu yake ilikuwa ya ajabu sana. Baada ya miaka michache ilihitimu maarifa ya kuimba kinyumenyume na kimbelembele. Aliweza kuimba kwa sauti nzuri na kwa utaratibu wa kupendeza kama kwamba alizaliwa mwimbaji. Isitoshe Kiarabu alichokuwa akitumia katika nyimbo zake kilikuwa na nahau kubwa sana.

Mwanamke huyu ambaye hakusoma, alikuwa na moyo wa kuhifadhi mambo upesi kama umeme. Kisha aliweza kuyakariri baadae neno kwa neno kwa namna iliyoshangaza kila aliyemsikia.

Baadaye, Siti alijiunga na jumuiya ya watribu maarufu sana wa wakati ule, Subeti Ambari; mpiga udi, Buda Swedi; mpiga gambusi, Mwalimu Shaaban; mpiga tari, na Mbaruku. Katikati ya wanaume hawa watano, mwanamke alikuwa mmoja tu, yaani Siti. Yeye ndiye aliyekuwa mwimbaji peke yake kati ya vinanda vyao.

Siti alikuwa hajui kupiga kinanda. Hakupata kujaribu mkono wake hata mara moja juu ya kinanda cha namna yoyote katika maisha yake yote. Walakini, sauti yake ilikuwa Zaidi ya kifani kati ya vinanda vya watribu. Ilifanya kazi ikashawishi kwa mvuto mwingi sana watu mbalimbali. Juu ya hilo, alizidi kujizoeza kuimba mpaka ilikuwa vigumu kumshinda kwa kuimba. Maji ya nazi yalikuwa yakingoja mvugulio. Sauti yake ilizidi kuwa nzuri kila siku ikaletea sifa jumuia yao.

Yeye alikuwa mwanamke wa kwanza katika Kisiwa cha Unguja aliyesabilia, akajitolea katika kazi kama ile ya starehe. Subeti, Buda, Shaaban na Mbaruku waliokuwa wakipata fedha kidogo kwanza walianza kulipwa fedha maridhawa sasa.

Kwa kadri sauti ya kinanda ilivyokuwa nzuri, lakini ile ya mwanadamu ilikuwa bora. Hilo lilimfanya Siti kuwa kama Johari katika jumuia ile. Alitia mvuto katika mioyo ya watu uliokuwa mgumu sana kupingika. Kila neno aliloimba lilikuwa kiungo cha mnyororo uliokusanya watu pamoja.

Kwa mnyororo huo alifunga wasikilizaji wake wasiweze kuondoka mpaka mwisho wa tamasha

Ilikuwa kazi nyepesi kufanya jumuia ya watribu. Kuinunulia vinanda kama udi au fidla, zeze au gambusi, filimbi au tari, na ala nyingine za muziki, lakini kufanya jumuia ile ilete fedha kulihitaji uwezo ambao Subeti,

Buda, Shaaban na Mbaruku walikuwa hawana.

Ilikuwa kazi rahisi vilevile kukaribisha watu kuhudhuria katika tamasha au tarabu, lakini kufanya watu wale kulipa fedha kwa onyesho walilofanyiwa kulitaka ushawishi maalum. jumuia yao ilikuwa tayari kununua ala zozote zilizotakiwa kwa muziki, lakini ala peke yake hazikutosha kulipa gharama ya tarabu wala kuvuta mtu yeyote kuzisikiliza. Watu walitaka mvuto. Mvuto wenyewe ulipatikana kwa Siti, mwanamke aliyekuwa mfinyanzi zamani.

Njia ya Siti katika Maisha ilikuwa si rahisi kwenda. Ilikuwa ndefu, sio fupi. Milima na mizunguko ambayo haikuonekana kwa macho ilimkabili. Hakufika katika ustawi aliokusudia pasipo kukutana na kikwamo. Kabla ya kufikia nusu ya ustawi wake alipambana na vikwamo kadha wa kadha. Ilimpasa kupigania njia yake kwa uchungu wa moyo na bidii ya mfululizo.

Katika siku yake ya kwanza alipopata nafasi ya kuimba katika tarabu iliyohudhuriwa na umati mkubwa wa watu, alitetemeka sana. Alipo potelewa na sauti yake nzuri. Ilivunjika kama kioo kilichoanguka chini ya sakafu. Alijikohoza kutakasa koo yake akajaribu kuimba tena na tena, lakini sauti yote iliyotoka ilikuwa kama mwunzi tu. Mwisho alitoka mbio katika tarabu.

Hilo lililegeza moyo wake, hakutokeza tena katika tarabu?

La, mara mia moja la!

Alikuwa katika mwanzo wa kujifundisha kazi yake. Kushindwa kwake katika siku ile kulichochea moto wa bidi iliyoendelea kuwaka mpaka mwisho wa Maisha yake. Kwa sababu aliona kama aliweza kutoa sauti iliyofanana na mwunzi, aliweza vilevile kutoa sauti ya kuimba. Kwamba kila aliyepiga mwunzi mwisho aliimba ilikuwa si kweli sana kwa mtu yeyote kuliko ilivyokuwa kwa Siti. Mtu kama huyu aliyekuwa na tumaini kama lile katika moyo wake, ilikuwa vigumu sana kutazamia kushindwa kabisa.

Siti hakufanikiwa katika kuimba kwa sababu alikuwa na kipawa kikubwa sana cha sauti kuliko watu wengi ambao hawakufanikiwa. Alifaulu kwa sababu alishikilia kazi yake kwa bidii na kwa muda wa siku nyingi. Kulikuwa na watu wengi walioshindwa kufanikiwa katika neno lolote, waliokuwa na vipawa vizuri na akili nyingi sana kuliko zake, lakini hawakuwa na ujasiri, dhamiri wala nia. Siti alifanya kazi ya kusulubika katika unyonge kwa muda mrefu, kisha akazuka katika heri katika dakika chache. Tena alidumisha ustawi wake mpaka alipochaguliwa kuondoka katika maisha haya.

Watu waliofikia kilele cha ustawi bila kazi na bidii kubwa walikuwa wachache sana katika dunia. Kama ungalihesabu jumla yao ungaliona kwamba isingalimaliza vidole vyako vitano vya mkono mmoja. Ustawi ulidharau mara kwa mara watu walioshindwa kujitengenezea ngazi ya kuufikia.

Jumla ya watu waliofika katika heri ya kushangaza kwa bidi kubwa na kazi ya mfululizo ilikuwa kubwa sana katika ulimwengu. Kama ungaliwahesabu ungalitaka makarani wengi na madaftarl makubwa kabisa. Siti alikuwa mmoja katika jumla hii. Kwa hivi yaonekana kama kwamba katika maisha yalikuwa na mapendeleo mengi sana kwa watu waliokuwa na ujasiri, nia na bidii ya kutenda mambo kuliko kwa wale waliongojea bahati tu.

Maisha yamejaa pingamizi mbalimbali. Siti angaliwezaje kufaulu kama asingalijaribu kuzishinda kama alivyotenda!

Hadithi ya Siti, binti wa baba mkulima na mama mfinyanzi, ambao hawakujua kitu kingine chochote katika dunia, isipokuwa dhiki chungu na

umaskini mkali, ilianza kuandikwa baada ya miaka miwili ya mauti yake. Kama haisadikiki sasa kama hadithi yoyote katika Alfu-Lela-Ulela ilivyo, sababu yake ni kwamba alionyesha uwezo na bidii kubwa sana kuliko ilivyotazamiwa katika maisha yake.

Aliishi maisha ya kukumbukwa milele juu ya pingamizi zake za ujinga wa kusoma, umaskini na unyonge. Hili lilikuwa jambo kubwa sana kwa mwanamke wa cheo chake. Alionyesha johari iliyowezekana kupatikana kwa mwanamke kama mila iliyomnyima ushirika iliwezekana kuhidiwa.

Wazo la kuhidi maisha yake katika mji lilikuwa moja katika zinduna kubwa kabisa alizopata kugundua katika dunia hii. Kama nuru ya wazo hili isingalimulika katika moyo wake, au kama angalifaidika kutumia nuru hii upesi kama ilivyowezekana, maisha yake yote yangaliishia katika miaka ya sahau, umaskini na dhiki, angaliona kwamba ilikuwa watu wengine siku zote, si yeye mwenyewe, waliokuwa wakipata fedha, ustawi, anasa na wingi wa faraja za maisha. Hili lilikuwa kweli. Kweli tupu kwa kadiri wasifu wake uliojaa mishuko ya tope na mainuko ya ajabu unavyojieleza wenyewe kwa watu.

Siti alikuwa si mmoja wa wahuni waliozoea kutoroka kwao wakakimbilia katika miji kukaa kama chaza juu ya mwamba, au kama kupe na mkia wa ng’ombe. Uzuri wa majengo mbalimbali ya mji mkuu wa kisiwa cha Unguja, pamoia na mchanganyiko wake wa ajabu wa lugha vilikuwa si vitu Vya mvuto wowote juu yake. Hakutaka kuwa kimelea cha mji. Alikuja mjini na kusudi maalum. Alitamani kufanya kazi pale. Na kama Watu wote waliokuwa na akili njema, hakupenda ustawi wake utokane na mapendeo yoyote. Alitaka utokane na ustahili wake mwenyewe. Mahali alipochagua kutenda tendo hili kubwa palikuwa hapa mjini. Mahali pengine popote palikuwa hapafai kwa tendo kama hili.

KUFAULU KWAKE TARABUNI

Siti alipotokea katika tarabu katika mara yake ya pili na baadaye, alionekana na mabadiliko makubwa kabisa. Zaidi ya kuweza kuimba alionyesha vilevile madaha na mtindo mpya uliochukua watu kwa ghafula, ukawatia katika mshangao rnkubwa. Ilikuwa vigumu sana kwa watu wale walioona kushindwa kwake katika mara ya kwanza, kusadiki kwamba alikuwa ndiye yeye kweli.

Sauti yake nzuri ilisikilika waziwazi, kisha kuimba kwake kiada kulijaa utamu na ufasaha uliowezekana kuchukuliwa na wasikilizaji wake mpaka kwao ukasimuliwa mara nyingi baadaye. Aliweza kuwapa kitu walichotaka sasa.

Jina lake lilianza kuvuma kama ngoma katika hewa, sifa yake ikaenea kama moto katika nyika kavu. Watu wa kila rika, wanaume na wanawake, katika vijiji na miji, katika vibanda na nyumba, toka visiwani mpaka mrima, kila pahali katika Afrika Mashariki, walishikwa na hamu ya kusimulia habari zake kwa shauku kubwa sana.

Ilikuwa uvumi mtupu?

Hasha! Ilikuwa si uvumi wa bure.

Palipokuwa na moshi, palikuwa na moto.

Siti mwenyewe alishangaa kwa yaliyomtokea. Alikumbuka kwamba alizaliwa katika unyonge uliokithiri. Fahari ilikuwa kitu kigeni kabisa kwake. Hakujua ilikuwa kitu gani. Kwa mzuko wake wa ghafula sana katika sifa, alijiona kama kwamba alikuwa akiishi katika maisha mapya katika nchi ya ndoto, iliyokuwa na mito ya maziwa na asali. Walakini, kweli ilikuwa kwamba aliishi katika ardhi hii hii ya majaribu, visasi na machozi. Isitoshe yale yote yaliyomtokea yalikuwa mavuno ya kazi ngumu na bidii yake mwenyewe. Utamu wa mazao ya jasho lake ulipozidi, naye

alizidi kufanya kazi kwa bidii vilevile. Mwendo wake ulikuwa kama huu siku zote.

Alihudhuria katika tarabu kadha wa kadha katika mji wa Unguja, akaimba mchana na usiku kama kurumbizi.

Bidii ya Siti haikukoma hapo. Alikuwa mtendaji aliyekuwa na uwezo na vipawa mbalimbali. Wakati mmoja alifungua natiki yake mwenyewe iliyodumu kwa muda ambao haukupungua miaka mitatu katika mji wa Unguja. Katika natiki hiyo aliimba akacheza mara kwa mara. Mchezo wake ulipendeza kama sauti yake.

Uigaji wa Siti katika natiki ulikuwa wa bahati tu. Haisemwi pahali popote kwamba alipata mafundisho maalumu juu ya kazi hii. Yamkini, siku chache alizokwenda katika sinema zilimtosha kumfanya mwigaji mwema. Alipata shangwe la watu wengi! Vigelegele vya hadhara nzima! Kutazama mwanamke katika majadi ya mchezo na kusikiliza miminiko la sauti yake katika wimbo yalikuwa mambo mazuri kabisa katika dunia. Mambo haya yaliyeyusha moyo wa mtu katika furaha isiyoelezeka kwa ulimi wala kalamu. Jicho halipepesi na sikio hutekwa.

Siti aliyekuwa mwanagenzi katika wanagenzi. Aliyetembea miguu wazi katika vumbi la ardhi. Aliyekuwa na kutuzi la shamba na nywele zilizofungika julfa kwa shida. Aliyetamka kulala badala ya “kila”, aliyesema “hafidhi” pahali pa “hifadhi”, aliyenena “jalili” alipokusudia kunena “jalali”, aliweza kustarehesha watu sasa kwa namna ya ajabu kabisa, ambayo haikupata kuonekana kwanza katika Kisiwa cha Unguja.

Mzaha ulitungwa ukaenezwa. Ilisemwa kwamba sauti ya Siti ilikuwa kama mtego wa mawindo, na natiki yake ilifanana na maangamizi tu. Kwamba alitaka fedha yote iliyokuwa katika mifuko ya wanaume. Afriti walijaza upuzi kama huo katika masikio ya watu, lakini haukufaulu mbele ya adili kubwa ya mwanamke huyu. Palikuwa hapana moja lililokuwa kweli katika haya yote. Siti alikuwa mwanamke mcha Mungu wa sala na saumu. Alisali vipindi vitano kila siku, akafunga faradhi na suna katika maisha yake yote.

Siti hakufanya natiki kwa sababu ya tamaa ya fedha. Kama fedha yote ilimjia kwa natiki yake ilikuwa kama baraka tu. Watu wachache sana waliokataa fedha katika dunia. Sababu hasa ya natiki yake ilikuwa kufurahisha watu waliopenda kupitisha wakati wao wa mapumziko katika tafrija kama ile. Alipenda sana kuona watu katika furaha kuliko alivyopenda kusikia mlio wa fedha iliyokuwa katika mifuko yao.

Hata kama madai kwamba Siti aliongozwa na fedha katika natiki au tarabu yangalikuwa kweli, ingalikuwa si aibu wala lawama kwake hata kidogo. Fedha ilikuwa jembe, la kulimia nafaka katika wakati wake kama ilivyo katika wakati wetu. Mtu yeyote hakuweza kutenda neno bila jembe hili la ajabu. Watu wengi bora kuliko alivyokuwa yeye, Watu wengi watukufu waliokuwa juu yake, waliuza nchi zao kwa hiana, watoto wa damu na miili yao kwa ulafi, hata watakatifu wao kwa utajiri. Historia na misahafu imejaa tele kweli kama hizi. Siti alitumikia watu kwa moyo mweupe. Hakutenda jambo moja katika mambo yaliyoaibisha uungwana kwa sababu ya faida yake mwenyewe. Kwa hivi, fedha yoyote aliyoweza kupata ilikuwa kama ujira wake wa haki na halali.

Yamkini utaona ibada na malimwengu vilikuwa vitu mbalimbali. Havikuweza kuwa pamoja kwa amani. Basi, mwanamke huyu aliwezaje kuvisuluhisha kudumu katika moyo wake bila ukinzani? Kwa hakika. mambo yalikuwa hivi: Siti alikuwa mtu wa ibada katika wakati wa ibada. Alikuwa mtu wa malimwengu kama watu mengine katika wakati wa ada za ulimwengu.

Kwa kila hali, alikuwa kama yule mtu mwerevu kabisa katika ngano aliyeweza kuvusha nyasi, mbuzi na chui kwa dau moja. Kama hii ilikuwa ila au sifa kwake, si kazi yangu kusema. Kazi yangu yote kama mwandishi wa kitabu hiki ni kujaribu kusimulia maisha yake kwa hesabu ya matendo yake na kwa usahihi wote uwezekanao. Kadhalika, mimi si kasisi wala sheikh wa kuamua kitu gani: ibada au malimwengu, kilikuwa kwa mtu?

Hapana mtu aliyechoka kumsikiliza Siti. Watu walipata faraja katika nyimbo zake zilizokuwa kama kioo cha kutazamia mioyo yao. Faraja yenyewe ilikuwa adimu sana kupatikana sokoni. Haikuuzwa wala kukopeshwa. Siti aliitoa bure kwa watu wote, isipokuwa alipata nauli alipotakiwa kuhudhuria katika tamasha iliyokuwa mbali, au zawadi mara

kwa mara kwa watu waliokuwa karimu. Kama kwa zawadi hizo aliweza kufanya rasilimali yo yote ilikuwa bahati yake tu, ilikuwa si chumo hata kidogo. Hakudai deni wala hakushtaki mtu kwa ujira wake. Alitumikia watu pasipo mkataba wa namna yoyote.

Palikuwa na watu waliotegemea sana masharti ya mkataba au mapatano katika kazi zao zote. Waliojali sana uhodari au uwezo wao wenyewe kuwaletea kila kitu walichotaka katika maisha, kuliko walivyohesabu neema za baraka au ukarimu. Siti ameacha fundisho la namna ya peke yake katika dunia. Alikuwa na uhodari na uwezo lakini hakutegemea mambo haya. Alitegemea sana neema za ukarimu na baraka kuliko alivyojali masharti ya mkataba au mapatano.

Una hiari ya kusema alikuwa mtu wa zamani, lakini utasita kunena alikuwa mjinga. Watu waliweza kuwa na kisa cha kubatilisha mkataba au makubaliano mazuri, lakini hawakuweza kupata sababu ya kutangua baraka au ukarimu kwa sababu chemchemi yake ilikuwa mbinguni. Haikuwa katika mikono ya wanadamu hata kidogo. Imani kama hii katika moyo wa mwanamke ilikuwa kubwa sana. Ilikuwa zaidi ya johari katika moyo wa mwanadamu.

Alitafutwa akaandamwa na watu kadha wa kadha sasa, kama kwamba alikuwa mmoja wa mabinti Sultani wa Unguja. , Kumbe alikuwa muimbaji tu ambaye hakujulikana na mtu kwanza. Watribu walimzunguka pamoja na vinanda vyao. Wapiga picha na wapiga chapa walimshugjulikia. Mafundi wa sahani za santuri walimkimbilia wakapata pesa nyingi sana kuliko ile aliyopata yeye. Waliweza kupata shilingi elfu moja hata zaidi kwa kila shilingi mia moja alizoweza kupata yeye. Fedha ilitiwa katika mifuko yao kama nafaka ilivyotiwa katika magunia. Picha zake zilitokea katika vitabu vya orodha za nyimbo pamoja na jina lake limeandikwa vizuri kwa herufi kubwa. Sauti yake ilienea katika santuri za ulimwengu.

Watu waliokuwa hawawezi kumwona yeye mwenyewe, walitafuta picha yake katika kila pembe ya Afrika Mashariki wakaitazama kwa kuiajabia sana. Walimimina fedha katika mifuko yao wakanunua vinanda. Biashara ya santuri pamoja na sahani zake ilizidi mara mia nyingi. Mia za santuri na elfu za sahani zake zilinunuliwa kwa thamani nzuri. Faida kubwa sana ilimiminika kama mto katika mifuko ya wafanyabiashara.

Maendeleo katika tarabu za Afrika Mashariki yalihimizwa sana na mwanamke huyu aliyetoka kijiji kidogo katika kisiwa cha Unguja. Kwa uwezo wake wa mwujiza aliweza kuchukua, kwa hatua kubwa, watu wa upande huu wa dunia akawatia katika maendeleo makubwa ya kuimba. Wangalikuwa nyuma miaka mingi sana kama asingalitokea mbele kama kiongozi akaonyesha kama waliweza kutumbuiza kama watu wa nchi nyingine.

Nyimbo za kiswahili unazozisikia leo katika santuri zingalichelewa sana kusikiwa na watu wote kama Siti asingalipata kuishi katika upande huu wa ulimwengu. Fedha ya waswahili iliyokuwa ikipotea bure kwa kununua vinanda kwa sababu ya mlio ambao hawakujua maana yake iliokolewa na majilio ya mwanamke huyu katika tarabu. Kama ulitaka sahani ya wimbo wake sasa, nadhani ingalikupasa kulipia thamani kubwa sana kuliko ilivyokuwa katika wakati wa maisha yake.

Ghairi ya sauti yake nzuri, mwanamke huyu alikuwa na utanashati uliovuta katika tarabu, umahiri wa kujizabuni mwenyewe kwa watu wote, na maarifa ya kupanga vizuri nyimbo zake mbele yao. Hakwenda katika tarabu yoyote pasipo kujipamba. Alipenda kuwa maridadi ijapokuwa katika mavazi hafifu. Kwa desturi hii aliweza kutumia alivyopenda ushawishi mkubwa sana kwa watu waliomwajabia. Ilikuwa kweli kabisa kwamba chema kilijiuza, kibaya kilijitembeza. Siti alivuta moyo wa kila mtu.

Jambo moja katika mambo niliyoajabia kabisa kwake, katika wakati tulipokutana kwa muda mfupi sana, lilikuwa kwamba mwanamke huyu hakuharibika kwa fanaka, sifa, fedha na watumishi waliolipwa mishahara kila mwezi katika nyumba yake. Alikuwa hama majivuno ya kuchukiza kama yale ambayo mtu alikutana nayo mara kwa mara kwa baadhi ya watu waliojidhania kuwa bora. Alikuwa na adabu na mlahaka kwa watu wote, kama alivyokuwa mnyonge katika miaka ishirini au thelathini iliyopita katika kijiji cha Fumba, alikomsaidia mama yake kupika jikoni, kusafisha vyungu na kufagia nyumba.

PINGAMIZI NA WIVU

Jina lolote kubwa halipatikani duniani bila vizuizi kadha wa kadha. Aghalabu, lilishawishi wivu na mashindano toka upande, hasa kama jina lenyewe lilihusiana na mtu aliyedhaniwa kuwa duni. Katika kuhesabu ubora wa mtu macho ya ulimwengu yalivutwa sana na fahari ya nasaba na miliki ya utajiri. Watu wachache sana waliona haki ya kuamuru ustahili wowote wa ubora kwa mtu duni. Wengi wao walikuwa na husuda ambayo haikuwa na sababu yoyote njema. Walitii wivu wao wakadunisha wanyonge hata kama walikuwa johari kwa matendo yao duniani. Kinyume chake kilikuwa kwamba ngoa mbaya kama hiyo haikufaulu. Wanyonge wengi sana waliweza kujitukuza sana wenyewe kuliko ulimwengu ulivyowatazamia.

Siti alipokuwa akiingia katika mlango wa sifa aliyostahili kwa kila hali, makelele ya pingamizi yalitokea pande zote. Alishambuliwa kwa dharau mbaya na matukano makali sana. Hakuhurumiwa na karaha wala jeuri. Alikuwa hana rafiki upande wa kulia wala upande wa kushoto. Hakuona msaada mbele wala nyuma. Washindani wake wakali walipotelewa na akili kwa wivu. Kila ila ya umbo ilikuwa shabaha ya matusi yao kama kwamba Siti alijiumba mwenyewe. Kwa nazaa kubwa waliimba kama hivi:

Siti binti Saad,

Ulikuwa mtu lini?

Ulitoka shamba,

Na kaniki mbili chini,

Kama si sauti,

Ungekula nini?

Upeo wa dharau juu ya mwanadamu ulikuwa kama huu. Hii ilikuwa kashifa tupu, si wimbo hata kidogo. Walioimba wimbo huu walikosa adabu idhaniwayo kuwa adili na johari ya mwanadamu. Kashifa kama hii ilitangazwa juu ya mtu bila mashtaka kwa sababu ustaarabu wa Afrika Mashariki ulikuwa katika mimba ya wakati ujao. Hatia hii ingalifuatwa na lawama kali katika nchi yoyote nyingine duniani. Wimbo huu ulidara watu ukaenea kama moto uliokuwa ukiruka na kuunguruma kwa ukali katika msitu wa misonobari. Kila upande ulileta watu kutazama sura ya Siti, kama kwamba uzuri wa sura ulikuwa ndiyo sababu kubwa kabisa kwa mwanadamu ya kupatia riziki yake.

Siti alivunjika moyo akalilia ardhi ipasuke, ajizike ndani yake futi elfu moja?

Mawe! Siti au mtu mwingine? Siti hakuonekana katika desturi ile.

Alikuwa si mwanamke wa kukata tamaa, akaonyesha saburi na uvumilivu wa ajabu.

Kwa desturi, mwanadamu alikuwa kiumbe wa ajabu siku zote. Alitukuka upesi kwa kudunishwa, kama alivyodhalilika mara moia kwa kutukuzwa. Hakutetea sana fahari yake, kuliko alivyotetea unyonge wake mara kwa mara. Ukidunisha mtu leo, utamwona juu ya kilele cha utukufu kesho. Dhila au dharau ililipua fataki ya utukufu katika moyo wa mtu mara kwa mara. Waivu wa Siti wangaliepuka mashaka mengi kama wangalimsifu badala ya kumkashifu.

“Asiyeweza kutuumba, kutuumbua hawezi,” ni methali moja maarufu sana katika methali za Kiswahili. *“Cheka uchafu, usicheke kilema* ni mfano wa pili wa maneno ulio sawa na wa kwanza kwa muhimu. Ingalikuwa heri kwa washindani wa Siti kama wangalifahamu maana ya maneno haya ya kawaida, lakini yenye hekima.

Maisha ya Shamba yalimpa Siti mwanzo mwema sana. Alikuwa na moyo mkuu. Hii ilikuwa si mara yake ya kwanza ya kujaribiwa. Dhiki kubwa na umaskini mkali vilikuwa vimekwisha mjaribu vikamfanya imara kama mwamba. Hakuchelea kauli ya watu waliosema mchana wakalala usiku. Alijua barabara kwamba riziki haikuletwa wala haikupingwa na sura nzuri au mbaya. Kwa kujitegemea mwenyewe kama hivi, aliweza kutimiza matumaini makubwa yaliyokuwa katika moyo wake.

Mahali pa kuchekwa kwa ubaya, aliajabiwa na watu wote waliokuja kumtazama. Masikio yao yalitekwa na sauti yake ya ajabu. Kila mtu alionekana kama kwamba alirogwa mbele yake.

Kama Siti angalisita kwa sababu alikuwa si mtoto wa mtu, au kichwa chake kilikuwa si mviringo, uso wake ulikuwa si mzuri, au hakuwa na nywele za kufunga julfa, hakuwa na macho ya kikombe, au nyusi zake zilikuwa si za kifungo, pua yake ilikuwa si ya mwanzi, au midomo yake ilikuwa si miteke, meno yake yalikuwa si meupe wala hayakuwa na mwanya, au Shingo yake haikuwa ya mbuni, hakuwa na kifua cha juu wala matiti ya dodo, au tumbo jembamba, hakuwa na miguu iliyoviringiana wala mwendo wa njiwa, angalipatwa na hasara kubwa sana.

Wazuri walikuwa na bahati zao, kadhalika wabaya walikuwa na vipawa vyao vilevile. Hapana mtu aliyeweza kubadili umbo lake, lakini palikuwa na watu wengi walioweza kujifaidia wenyewe kwa kukuza vipawa vyao vingine. Kama Siti alikuwa si mmoja katika wale waliokuwa na sura jamali, alikuwa mmoja katika wale waliokuwa na vipawa vingine vizuri.

Washindani baada ya washindani, wanaume kwa wanawake walimkabili Siti. Kila mwimbaji aliyesifika alipolinganishwa na Siti alikuwa si kifani chake. Katika wakati wake hapakutokea mwimbaji hata mmoja katika Afrika Mashariki aliyeweza kumshinda kwa kuimba, isipokuwa Umi Kulthum wa Misri.

Ajabu akidi hapa ilikuwa kwamba mkutano wa waimbaji hawa wawili haukujulikana pahali ulipokuwa. Walakini, ungamo kama hili ambalo lilipatikana kwa Siti mwenyewe, limeonyesha ushahidi wa moyo wake wa haki juu ya sifa za watu wengine.

Jina hili Siti maana yake ni bibi. Siti hakuwa bibi tu katika mabibi, lakini alikuwa malkia vilevile wa waimbaji katika Afrika Mashariki. Sauti yake nzuri haikupungua utamu Wala mvuto, hata alipokuwa amekwisha pita umri wa miaka hamsini.

Katika ulimwengu, kila mtu aliyeacha wazi masikio yake akasikiliza sana ila yake kwamba ilikuwa zuio la maendeleo hakupata faida. Hakuweza kuendelea hata kidogo.

Falau, Siti asingalitoka ufichoni, kule kijijini, akaja mjini, asingalitenda kama alivyotenda, angalisikiliza upuzi wa watu ambao hawakutenda neno, hawakubuni neno, hawakushauri neno, hawakujaribu neno, isipokuwa walikaa kitako wakadharau waliotoka ufichoni, waliotenda, waliobuni, waliofikiri, walioshauri, na waliojaribu, ambao walikuwa nyuki wa asali ya maisha, ingalikuwa hasara isiyo kadiri kwake.

Uzuri wa sura ulikuwa aula kweli, lakini ulikuwa si ufunguo wa kila heri. Ubaya wa sura ulikuwa dhila si uongo lakini ulikuwa si zuio la maendeleo. Watu waliishi duniani kwa matendo yao sio kwa sura zao. Matendo ndiyo yaliyowatukuza au yaliyowadunisha.

Kwa upande mmoja maumbile yalikuwa bahili kwa Siti. Hayakumpendelea kwa kumpa sura nzuri ya kuvuta wachumba matajiri kumwoa, lakini kwa upande mwingine yalikuwa karimu sana kwake. Yalimpa sauti nzuri ya kutosha kutumbuizia. Kwa utumbuizo wake aliweza kushawishi ukarimu wa matajiri kumlipa vema kwa kazi yake. Yalimhini kweli kwa uzuri, lakini yalimfadhili mara nyingi zaidi kwa mambo mengine yaliyokuwa azizi.

Yalimpa mabadiliko makubwa katika maisha. Kwa mabadiliko hayo aliweza kuinuka juu ya watu waliokuwa kama yeye.

Malezi makubwa ya wanawake katika nchi hizi yalikuwa utawa. Utawa huu ulifuatwa na mashindano ya ndoa kwa uzuri wa sura. Malezi haya yalikuwa mazuri, lakini hayakuacha nafasi ya matukio yaliyoweza kutokea kwa mwanamke kwa ujane au talaka. Nje ya ndoa wanawake

masikini walikuwa hawawezi kujitegemea. Kanuni hi ililazimu kuhidiwa. Kama Siti alikuwa na kusudi hili alipojitia katika kazi ya kuimba alikuwa mmoja wa wahidi wakubwa wa maendeleo ya wanawake katika Afrika Mashariki.

Utawa wa wanawake waliokuwa hawajui kufanya kazi yoyote ulikuwa si utawa wa aushi. Utawa wao ulilegea mbele ya maafa ya ujane, talaka au uzee. Iliwalazimu kuuza kitu bora kwa thamani hafifu sana. Waliuza maisha, roho na miili yao mara kwa mara kwa chakula, nguo au anasa za kitambo, badala ya kuuza kazi zao. Ilikuwa aibu tupu. Kama walijua kazi yoyote ya kutenda, aibu kama hii ingaliuzwa kabisa. Fahari moja kubwa kabisa katika fahari za dunia ilikuwa kuoa mke mtawa, lakini mtawa aliyekuwa hawezi kujitegemea katika nyakati za dhiki, alikuwa bure ghali kwa mwanamume, katika maisha na katika jinsi yake vilevile.

Katika maisha ya haraka, saa ishirini na nne, miezi kumi na miwili, na yaliyojaa gharama nzito wakati wote, utawa ulikuwa mchezo usio faida, isipokuwa ulisaidia biashara ya kitambaa cha buibui dukani. Uliviza fikira, akili, adili na bidii ya mwanamke, ukamfanya windo jepesi la shetani katika dunia ya dhoruba kali na mashaka mchana na usiku.

Kama si sauti angalikula nini, ilikuwa kweli sana kwa Siti kama kusema mchana ulikuwa na nuru na usiku ulikuwa na giza. Ilikuwa si uongo kwa mwanamke yeyote mwingine aliyekuwa hana tegemeo jingine Zaidi ya sura yake. Kama mtu, mwanamume au mwanamke, hakufanya jitihadi ya kutimiza mradi fulani aliokusudia, maisha yake yalikuwa hayana maana hata kidogo. Kila mtu ilimpasa kukisi tena na tena kama alitaka kufaulu rasi ya mafanikio katika maisha yake. Maisha yalikuwa kama merikebu, na mtu alifanana

na nahodha wa kuongoza merikebu ile katika bandari ya ustawi, haidhuru kwa hali yoyote, mbele ya tufani au shwari, mbele ya giza au mwangaza.

Faida aliyopata Siti kwa kuimba ilikuwa zaidi ya maridhawa. Mwanamke huyu huyu ambaye hakuwa na nyumba ya kukaa, pambo la kujipamba wala nguo nzuri za kuvaa zamani, aliweza kujinunulia nyumba mbili nzuri, mapambo nakawa ya kujipamba, libasi teule za kuvaa, na tunu au faraja

nyingine zilizopatikana kwa fedha sasa. Haya yote yalikuwa mazao ya kazi yake.

Ukipenda waweza kuita ustawi wake ajabu, lakini kwa kweli ilikuwa si ajabu hata kidogo. Siti alifaulu kwa sababu alikuwa tayari siku zote kushindana katika holi ya maisha.

Laiti fahari isingaliingia katika kichwa chake, kama ilivyozoea kuingia vichwa vya wanawake wengi mara kwa mara, asingalikuwa mbadhirifu katika anasa za kufilisisha, rasilimali yake ingalikuwa kubwa sana. Angaliweza kukusanya shilingi laki tano, sio shilingi elfu tano, tazama, shilingi laki tano! Jumla kama hii ya fedha ilikuwa kubwa kabisa ambayo imepata kupita katika mikono ya mwanamke yeyote Mwafrika katika Afrika Mashariki. Hili lilikuwa kama pato Ia shilingi kumi na tatu elfu kila mwaka katika miaka ile thelathini na tisa ya maisha yake ya kuimba.

Baada ya kusema kila neno katika sura hii, hapana kitu kilichomfaulisha sana Siti katika maisha yake kama mwimbaji bora isipokuwa waivu wake wakali. Mara alipowashinda alikwenda kwa hatua kubwa moja kwa moja katika heri iliyokuwa ikimngojea. Cheche ya kipawa katika sauti na uigaji wake haikung'aa mpaka alipotangazwa kwa wivu ule mkali.

Tokea pale na baadaye, binti

huyu wa mkulima maskini wa Fumba alishawishi bahati kubwa kumwandama. Bahati yenyewe ilikuwa kubwa ya ajabu. Aliogelea juu ya wimbi la jaha baada ya wimbi la jaha kwa upesi wa kufumba na kufumbua kope. Alifululiza kufanya hivyo mpaka akafikia ustawi ulioshangaza wasifu wowote wa mwanamke katika Afrika Mashariki.

Bidii za kawaida au wastani zilikuwako daima, lakini bidii kubwa kabisa, kama zile zilizoacha nuru au alama katika dunia hii, baada ya mauko ya wale walizozitenda, zilipekechwa mara kwa mara na dharau mbaya, wivu au mashindano makali katika moyo wa binadamu.

JAWABU AMBALO HALIKUTAZAMIWA

SITI binti Saad hakuridhika kuishi bila mwongozo kama mnyama. Akuwa na ramani ya namna fulani ya kumsaidia katika maisha yake. Ramani yake ilikuwa "Kusema fedha, kujibu dhahabu." Kwa ramani hii ya maneno manne mepesi sana, lakini ya adili kubwa, aliweza kupambanua jema au baya, sifa au kashifa katika safari yake. Pasipo ramani, ijapokuwa ndogo, safari katika maisha ilikuwa si nyepesi. Dhana au kisio lilikuwa si zana ya kutosha katika safari kubwa ya maisha ya mwanadamu. Majaribu ya maisha yalitazamiwa kumtokea katika wakati wowote. Ilimpasa kujiweka tayari kukutana nayo kwa kujua jinsi ya kutenda bila kupoteza wakati. Maisha yalikuwa si marefu ya kuamuru usiri mwingi.

Katika maisha watu walikuwa kama wasafiri waliokutana katika nchi ngeni iliyokuwa bado kugunduliwa wakalinganisha usahihi wa maelezo mbalimbali ya ramani zao. Baadhi ya ramani zilitengenezwa kwa ustadi na maelezo yake yalikuwa sahihi. Nyingine zilikuwa na makosa zikasahihishwa wakati wa kulinganishwa. Tutazame kama ramani ya Siti ilikuwa sahihi au sivyo. Alipojitetea juu ya shambulio la waivu wake, jawabu lake lilikuwa hili:

Si hoja uzuri

Na sura jamali,

Kuwa mtukufu

Na jadi kubeli,

Hasara ya mtu-

Kukosa akili.

Jawabu kama hili kutoka kwa mtu wa malezi madogo kama Siti ilikuwa Zaidi ya ajabu iliyotazamiwa na watu. Lilikuwa si jawabu latifu tu. Lilikuwa jawabu la kiungwana kabisa, vilevile lililoweza kupatikana kwa mwanadamu aliyekuwa katika joto lisilovumilika la dharau na karaha. Waivu wake walitazamana wakashangaa sana. Nyuso zao zilishuka kwa aibu. Fadhaa ya kushindwa ilikabili macho yao. Kila mwivu alitafuta pembe ya kuficha uso wake. Siti alipata zawadi ya ushindi kwa jawabu la dhahabu alipokuwa katikati ya nazaa ya maisha yake.

Zihi ya maisha ilikuwa katika mashindano. Bila mashindano maisha yalikuwa dufu. Pasingalikuwa na maendeleo ya namna yoyote. Pangalikuwa na kuishi na kuondoka bila jina moja katika mashajara ya watu.

Nazaa juu ya Siti ilikuwa kali, lakini ilikuwa nje ya msingi. Jawabu la Siti lilikuwa pole, lakini lilikuwa juu ya msingi imara. Miliki bora kabisa ambayo ilikuwa sehemu ya busara. Pili ilikuwa uzuri, na elimu ya kutafutia kweli. Siti aliposema kwamba hasara ya mtu ilikuwa kukosa akili, yaani, busara ilikuwa kweli kabisa. Kwa wimbo huu wa mistari sita mifupi, mwanamke huyu aliyedharauliwa, aliweza kusema kweli ya kuishi milele.

Siti ameacha wimbo mwingine ulioshinda purukushani yangu. Nimejitahidi sana kujipurukusha kuacha kuudondoa katika wasifu wake, lakini sikuweza.

Wimbo wenyewe ulikuwa huu:

Si kusudi langu,

Kuvunja watani,

Enyi walimwengu,

Mwajua yakini,

Apendalo Mungu,

Haliwezekani.

Katika wimbo huu twapata jawabu lake la pili bora. Alitamka jawabu hili alipojibu mashtaka ya lawama kwamba aliumbua uzuri na ubora wa nasaba kwa wimbo wake kwanza. Sijui jawabu gani jingine lililoweza kusadifu zaidi ya hili! Ilikuwa ibra iliyotosha kufahamisha watu mwanamke huyu alikuwa nani. Alikuwa mtu mashuhuri kweli.

Ijapokuwa nyimbo hizi mbili zilikuwa fupi, lakini udhahiri wake ulikuva mkubwa sana. Tazamo moja katika mistari hii ilitosha kumpa mtu muhtasari wa waziwazi juu ya dhamiri kubwa na tabia bora kabisa ya mwanamke huyu. Katika uchungu wa matusi makali mwanamke huyu hakufadhaika. Alikuwa na utawala kamili juu ya ulimi wake. Hakusema ovyo kama mwenda wazimu. Alikuwa mteuzi wa maneno na fikira. Adabu katika kusema ilikuwa sawa na johari adimu kwa mwanadamu. Nusu ya ustawi wa

Siti ililetwa na vitu hivi viwili vyema katika kujitetea kwake.

Dhamiri njema katika moyo huweza kuamsha hata dufu la mtu kama Siti alivyokuwa, ikampa uwezo mkubwa wa kusema na kuzusha maoni ya kufikirika. Mwanamke huyu alipokuwa katika majadi ya dhamiri kama hiyo alisema lugha ya mashairi ya shani kubwa katika nyimbo zake zote.

Baadhi ya watu waliona rahisi kufanya ufidhuli ulioweza kuumua dunia nzima katika hasira kali, lakini yake yalikuwa majuto makubwa vilevile. Watu wengine waliona vigumu kufanya adabu kama kwamba ilinunuliwa ghali dukani, lakini matokeo yake yalikuwa ushindi wa kiungwana daima.

Siti hakuweza kuacha kujitetea. Ilikuwa si desturi ya mwanadamu kuacha maangamizi ya salama yake. Heshima yake ilikuwa katika hatari. Lakini alikuwa mstaarbu barabara. Hakujitetea kishenzi kama mnyama wa porini.

Tua yake ilibadilika kwa nyimbo hizi za kupendeza. Zilikuwa nzuri sana zikamfanya kuwa mashuhuri badala ya kuwa duni mbele ya washindani wake.

Kwa kuwa hapana mtu mwingine aliyeweza kusawiri tabia ya Siti kwa ufupi wa kufahamika na ukamilifu mwingi sana kuliko alivyofanya Mwaalimu Shaaban, sina budi kuungama kwamba purukushani yangu yote ya kuacha kudondoa maneno yake hapa imeshindwa tena. Alifuatana naye kwa muda mrefu uliompa nafasi ya kumfahamu vema. Mwalimu Shaaban aliimba kama hivi:

Siti wa sitawa

Na umaarufu,

Na wingi wa haya

Na ujamilifu,

Pokea hedaya

Ingawa dhaifu.

Sanamu halisi ya tabia ya Siti, mwimbaji aliyepata sifa, shangwe na vigelegele vya kila mtu, kundi na umati wa Afrika Mashariki nzima kwa sababu ya ustahili wake uliokuwa hauna kifani, imepatikana katika wimbo huu mdogo. Mwimbaji huyu alithubutu waziwazi ustawi na umaarufu wa Siti kwa mkazo wowote mwingine, wimbo huu mmoja ulitosha kushuhudia ubora na uanadamu wa Siti.

Kila neno, jema au baya, ambalo mtu hulipata katika dunia hii, lilikuwa kama hedaya yake. Kwa desturi, hedaya tamu zililaza watu katika usingizi mzito, wakati zile chungu zilipowaamsha wakachimbua johari adimu zilizojificha katika mioyo yao.

Wimbo ule wa mzaha kama ya

kuvaa kaniki ulikuwa si dharau ndogo kwa Siti. Mtajo wa sura yake mbaya ulikuwa hizaya kubwa vilevile. Hatujui michomo gani michungu ilifuma katika moyo wake katika wakati ule wa majaribu. Kawaida ya maumbile juu ya utajiri na umaskini, na juu ya sura mbalimbali za wanadamu haikuhesabiwa kabisa na washindani wake. Wajinga walikuwa wakiumbua hali waliokuwa hawawezi kuibadili na kitu walichokuwa hawawezi kukiumba. Ilikuwa jeuri kubwa akapigana nayo kwa uwezo wote aliokuwa nao. Pigano lake halikumfanya kuwa mwimbaji bora wa wakati wote katika Afrika Mashariki tu, lakini lilimwongoza vile vile katika uchaguzi wa fikira kubwa na matumizi ya maneno yaliyojaa maana na kweli. Dharau ilikuwa zuio baya kwa mtu ambaye ilimshinda, lakini kwa upande mwingine, ilikuwa msaada mkubwa sana kwa yule aliyejaribu kuishinda kama Siti alivyotenda. Kwa hivi, mwanamke huyu aliweza kujipatia furaha ya kutosha katika dunia hii iliyokuwa imejaa ubahili, pingamizi na dharau wakati wote.

Iliwezekana kujenga ukuta kuzunguka bara na bahari za ulimwengu kama Mfalme Mkuu wa Dunia alitaka. Ukuta wa namna hii ulikwisha jengwa katika nchi ya Sina tangu miaka mingi sana iliyopita. Lakini haijawezekana wala haitawezekana kujenga ukuta kuzunguka kinywa cha salata. Kinywa cha mtu kilitaka hekima ya kukizuia kupayuka ovyo. Siti alikuwa na busara ya kuzuia watu waliopayuka ovyo juu yake. Aliweza kutimiza hilo kwa uvumilivu mwingi na dhamiri kubwa.

Siti hakupata kujidai hata mara moja kwamba alikuwa mwimbaji hodari peke yake katika Afrika Mashariki. Utumbuizo na uzuri wake vilikuwa vitu vilivyojulikana katika nchi hizi kabla ya kuzaliwa kwake. Basi, kama palikuwa na watu wengine walioweza kuimba vema kama alivyofanya yeye, siri ya ustawi wake ilikuwa nini?

Ustawi wake ulitokana na sababu mbili, nazo zote zilikuwa si ndogo. Kwanza, alifahamu sana tabia ya watu. Adabu yake ilikuwa kubwa, kisha alijua kuchukuana nao. Mambo hayo yalikuwa muhimu sana kwa mwimbaji. Kila tendo alilotenda, hata matamko ya sauti na matazamo ya macho yake yalikuwa yamekwisha andaliwa mbele. Kwa mfano, alijua kwamba mvuto wa sura yake ulivyokuwa. Kwa hivi, shabaha yake kubwa

ilikuwa kushawishi masikio, mioyo na fikra za watu badala ya macho yao. Ushawishi wake katika sikio, moyo na fikira ulifauluje? Kwa kuchelea kuudhi macho ya watazamaji wake waliopenda sura nzuri, alipoimba alizoea kujifunika gubigubi kwa utaji mzuri. Katika hali hiyo ya kujifunika, nguvu ya sauti yake haikuhinikizwa hata kidogo. Mfano huu si mkubwa wa kutajwa hapa, lakini ni mkubwa wa kutosha kuonyesha jinsi mwanamke huyu alivyokuwa tayari siku zote kukalifu nafsi yake mwenyewe ili watu wengine wapate furaha yote aliyoweza kutoa.

Na pili, alipenda sana hadhara yake akajishughulisha huku na huko. Kabla ya kuanza kuimba aliamkiana akashikana mikono na watu wote kwa ucheshi. Ilimpasa kuwakaribisha vema. Alikuwa na kazi ya fahari. Alikuwa katika furaha ya kazi yake. Ilimlazimu kuwaitia katika shirika ya furaha yake. Alielewa kwamba kama yeye mwenyewe alikuwa hana furaha, basi isingaliwezekana kwamba mtu mwingine angaliweza kupata furaha yoyote katika hadhara ile. Alikuwa mtu wa mrua mkubwa. Kwa mrua kama huo, aliweza kupanda daraja baada ya daraja ya ustawi ulioajabiwa sana.

Kwa kuwa Siti hakupata kwenda chuoni kama ilivyokwisha elezwa katika kurasa za nyuma, hapana shaka alikuwa na upungufu mkubwa elimu. Lakini kwa sababu nyingine, ukiangalia mambo aliyotenda utaona kwamba mwanamke huyu alikuwa bingwa, ijapokuwa alikuwa maskini wa elimu idhaniwayo kuwa uwezo mkubwa kwa mwanadamu katika dunia. Aliweza kuona mbele akajiandaaa, alijua mengi akaficha mengi yaliyopasa kufichwa.

Wakati wa usichana wake kule kijijini, hakushughulikiwa na mtu yeyote, lakini hakujali. Wasichana wenziwe walimwita mjinga mkubwa alipohama kijijini kwao, lakini hakughairi. Jaribu lake Ia kwanza katika tarabu halikufaulu, lakini hakufikiri habari ya kukata tamaa. Washindani mbalimbali waliokuwa na dhamiri ya kumshinda walimganda kwa wivu kama mchezaji stadi alivyogandwa na maadui katika shindano la mpira, lakini hakulegea. Umbo lake liliumbuliwa kwa kashifa kubwa, lakini alikuwa na kitu kingine cha kutoa kwa watu, aliwapa sauti yake. Mwisho, aliweza kuingia katika umashuhuri. Watu kadha wa kadha walimtafuta wakamwandama na kofia mikononi ili wapate kusikiliza sauti yake nzuri.

Alijaliwa kuishi akaona wasichana wale waliompuza kwanza wakidai sasa fahari kwamba walikuwa wenziwe na marafiki zake bora.

Ingawa alikuwa katika upeo wa umashuhuri wake sasa, lakini hakusahau ilikuwa nini kuwa mnyonge, ijapokuwa aliajabiwa na watu kadha wa kadha, alijua taabu gani ilikuwa kushindania ustawi katika dunia. Hakujisifu mwenyewe hata mara moja. Alikuwa mtu mnyenyekevu siku zote, ijapokuwa alikuwa mashuhuri katika Afrika Mashariki.

MABADILIKO YA HERI

SITI alipoimba wimbo wake wa kwanza wa kujitetea katika tarabu, kama ilivyoonekana katika kurasa za nyuma, miguu yake ilianza kukanyaga juu ya kizingiti cha umaarufu tokea siku ile. Ilikuwa fanaka kubwa ya maisha yake iliyopatikana kwa dhoruba moja.

Nyimbo za Kiswahili zilikuwa tunu. Zilikuwa bado kutokeza katika tarabu. Majilio yake yalitetemesha tarabu kwa hamu. Ilikuwa hamu ya kila mtu, fahari ya lugha na ari ya Afrika Mashariki nzima kuwa na nyimbo kama hizo. Wakati wa ajabu ulikuwa mbele ya watu. Siti aliyekuwa amekwisha jiandaa, aliogelea katika mkondo wa majilio yale mpaka alifikia umaarufu kama ule ambao hakutazamiwa kuupata. Turufu ilikwenda kwa mchezaji siku zote, nayo ilikwisha kuwa katika mikono ya Siti.

Tangu wakati ule alipata makaribisho mengi sana kuliko yaliyopatikana na mtu mwingine yeyote katika Afrika Mashariki. Laha kadha wa kadha za karatasi zilimalizwa kwa kumualika Siti. Barua na simu zilimpukutikia kama majani ya miti katika wakati wa kipupwe. Alikaribishwa na wateule wote wa Kisiwa cha Unguja. Watribu na washairi walimshangilia kama mwimbaji bora kabisa wa wakati wake. Jina lake lilikuwa mazungumzo ya watu wa nyumbani.

Kama Siti asingaliimba wimbo ule, bila shaka, umaarufu wake wa ghafula usingalifika katika masikio ya walimwengu. Wimbo ule ulipumbaza watu ukawafanya wamesahau kabisa habari za zamani za mwimbaji huyu. Walidhani walikuwa mbele ya mwimbaji wa waimbaji. Alikuwa si msichana tena wa kijijini aliyekuwa akipata riziki yake kwa ufinyanzi. Alikuwa mwimbaji mkubwa. Badala ya kuuza nguvu zake alikuwa akiiuza sauti yake

sasa.

Mwujiza huu ulikuwa si mdogo. Ulikuwa mwujiza uliofuatwa na badiliko kubwa sana la maisha yake. Badiliko hili lilifanywa na mtu mwingine?

Hasha. Lilitendwa na mwanamke huyuhuyu aliyekuwa mfinyanzi tu katika ujana wake wote.

Alighani katika tarabu kwa muda wa miaka thelathini. Kila siku aliweza kuimba nyimbo ambazo hazikupungua kumi na mbili kwa saa katika siku moja. Idadi ya nyimbo zake katika mwaka mmoia ilikuwa ni zaidi ya nyimbo elfu nne. Jumla hii ilitosha kuwa kitabu cha maneno laki moja, kama kila Wimbo ulikuwa na maneno thelathini. Kama nyimbo hizo ziliandikwa, hapana shaka, mwanamke huyu angaliweza kuacha kadiri ya vitabu thelathini vikubwa katika mauko yake.

Katika shindano lolote la kukariri, mwanamke huyu alikuwa hana mwenziwe. Nafasi zake za kushinda zilikuwa tisini na tisa kwa mia. Aliweza kukariri nyimbo kubwa na mashairi marefu baada ya kuyasikia mara moja tu. Upungufu wake mkubwa ulikuwa kutojua kusoma.

Siti alikuwa na kinywa cha mbubujiko mkubwa wa muziki, na sauti yake ya ajabu ilitumbuiza daima kama chemchemi ambayo haikufikiwa na kiu. Alikuwa na uwezo vilevile wa kuonyesha watu alikuwa akiimba nini. Masikio na mioyo ya watu wote katika tarabu vilikuwa kama vitu vilivyokuwa katika mikono yake. Mahali pa kufinyanga vyungu, alikuwa akifinyanga furaha katika mioyo yao.

Ukikosa uta na mshale hufumi kilicho mbele. Sababu mbili zilizopunguza hazina iliyoachwa na Siti kwa Watu wa Afrika Mashariki zilikuwa kutojua kuandika na ukosefu wake wa msaada wa mwandishi. Alikuwa na sauti aliyoweza kuieneza alivyopenda katika katika hewa ya ulimwengu, lakini alikuwa hana kalamu ya kuandikia nyimbo zake ziwe kama urithi wa milele katika dunia.

Maisha ya watu wachache sana yalionyesha mabadiliko mbalimbali kama yalivyoonekana katika maisha ya Siti. Kwa mabadiliko hayo, alipata akili, huruma, upendo, na maoni. Mambo haya yalikuwa fani kubwa kwake. Yalisaidia kutia ladha fulani katika sauti yake iliyosisimua mioyo ya umati wa watu. Kama ungalipata kumsikia alipoimba shairi la Sultani Mfawidhishwa Khalifa bin Harub katika siku za fahari yake, lazima ungalisadiki kwamba kitu fulani cha ajabu kilikuwa katika sauti yake. Shairi lenyewe lilikuwa hili:

Umetutoka ushiridu

Dua lahu adhima,

Kurejea El Amiri

Sultani mwadhama,

Jamii twamshukuru

Mola Hayu El Kaima,

Astahaki salama

Maulana El Amiri.

Maulana El Amiri

Astahaki salama,

Na taabu ya bahari

Ya mawimbi na mrama,

Takuhafidhi fahar

Kula safari daima

Astahaki salama

Maulana El Amiri.

Bwana Ibun Harub

Ndiwe wetu mkarama,
Rabi akupe hijabu
Pasi adui kusema,
Yawe yako matulubu
Ishi mutakima,
Astahaki salama
Maulana El Amiri

Rabi atakunusuru
Unusurike imama,
Pasiwe wa kukudhuru
Hadi siku ya kiyama,
Hasidi mtaraghama,
Astahaki salama
Maulana El Amiri.

Bwana ulipoondoka
Raia tuliinama,
Sote tulidhoofika
Tulihadhiri jasama

Na sasa umefika

Mwili utarudi nyama

Astahaki salama

Maulana El Amiri.

llahi atakuhafidhi

Hifadhi ilo timama,

Utakalo ufawidhi

Adui akitazama,

Kwa kula heri ukidhi

ljunahi el Islama,

Astahaki salama

Maulana EI Amiri

Rabi mzidishe hadhi

Yastatii makama,

Umuondolee maradhi

Milele awe mzima,

Kwa baraka za ibadhi

Jududi zake karima,

Astahaki salama
Maulana El Amiri.

Yeye na wake jibli
Wende janati Naima,
Abdallah jalili
Said muhtarima
Maulana el Fadhili
Atabdui shamshama
Astahaki salama
Maulana El Amiri.

Tamati nahitimisha
Ndiyo mwisho wa nadhama,
Rabi akupe maisha
Wewe na wako ghulama,
Hapa bahati imekwisha
Nahofu Wako kalima
Astahaki salama
Maulana El Amiri.

Siti hakuajabiwa kwa sababu ya sauti nzuri peke yake, lakini sababu alifululiza pia kuimba. Kila alipotazamiwa kwamba atakoma, aliendelea kuimba. Kama wewe wadhani kwamba hiyo ilikuwa si kazi ngumu-ijaribu!

Mwanamke huyu hakuishi katika namna moja ya maisha kama wanawake wengi sana walivyokuwa. Aliishi katika maisha ya namna mbalimbali. Alikuwa msichana, mfinyanzi na mwuza vyungu katika kijiji, baadaye akawa mwanamke, mwimbaji na mwigaji katika mji. Alikuwa mtu wa dunia na dini. Katika wakati huohuo alikuwa mke, mama na msafiri. Mwanamke huyuhuyu aliyetetemeka, huyu huyu aliyepotelewa na sauti kwa haya siku chache tu zilizopita, alionekana amekaa imara sasa akiimba kama mtu wa picha katika tarabu ya picha. Haya yalikuwa si mabadiliko machache wala kidogo. Yalikuwa mabadiliko mengi na makubwa sana kwa mtu ye yote wa kawaida katika wakati wake. Haya yote yalitokea katika maisha yake ya miaka korija tatu na nusu tu.

Siti alijulikana kama mwimbaji mkubwa, lakini alikuwa hana maarifa mengi ya tarabu. Watribu waliomzunguka wakati wote walijua sana maarifa haya. Lakini yeye alikuwa na akili ya kujichanganya nao akawatia chonjo ya kuzidi kupiga vinanda. Hiyo ilikuwa sababu yake nyingine ya ustawi wake katika tarabu.

Mapema katika jaribu lake la kuwa mwimbaji, Siti alionyesha mapenzi ya ushirika au umoja. Mara baadaye alivuta watribu bora wa Unguja kuwa pamoja naye. Alisema kwamba alitaka kuwa mwenzao kama aliweza kupata nafasi kati yao. Ilikuwa rai nzuri sana kwake. Rai hii ilifanya kazi kama uchawi. Hakuhini ahadi yake. Aliiheshimu kama kiapo.

Kama mti ulikwenda kwa nyezo, mtu alitaka rai katika maisha yake. Rai ya ushirika au umoja ilikuwa moja katika rai bora kabisa katika maisha ya mwanadamu. Mtu yeyote aliweza kuona uanadamu na usawa katika rai kama hii.

Fahari ilikuwa mateso. Ilichochea mtu katika majaribu baada ya majaribu magumu, katika matendo baada ya matendo mbalimbali, na katika

mabadiliko baada ya mabadiliko mapya. Wakati uleule ilimzuia kutenda mambo aliyozoea.

Siti alitamani kupika chakula katika chungu alichofinyanga kwa mikono yake mwenyewe, lakini alikuwa hana nafasi ya kufinyanga udongo sasa. Kazi nyingine muhimu ilikuwa mbele yake. Alitaka kufurahisha watu waliokuwa wakingoja kusikiliza sauti yake tamu katika nyimbo mbalimbali. Hakuweza kuthubutu kuwaudhi. Kwa hivi, ilimpasa kupika chakula chake katika vyungu vilivyofinyangwa na watu wengine, ingawa alikuwa hapendi kuvitumia. Jambo hili lilikuwa sahala, lakini kwake lilikuwa takilifu kubwa. Tazama nguvu ya mazoea! Siti alikumbuka ufinyanzi wakati alipokuwa anatembea mapana na marefu katika nuru ya umashuhuri.

Mabadiliko yake katika maisha yalikuwa kama haya, na fahari yake ilikuwa kama hii, lakini mambo haya yote yalikuwa mamoja kwake. Hayakuvimbisha kichwa chake. Makuu ya kuchukiza yalikuwa mbali naye. Alikuwa mtu kama watu wengine. Alijipendeza kwa watu kama walivyojipendeza kwake.

Siti alikuwa mmoja wa watu walioishi katika dunia ya ushirika wa wanadamu. Alipenda sana watu kuliko alivyopenda umashuhuri wake mwenyewe. Hakujali kama baada ya mauko yake, palipandwa mbono au paliweka jiwe kama alama ya kuonyesha malazi yake ya mwisho, ingawa alikuwa mwimbaji mashuhuri aliyeweza kujaza umati wa watu katika tarabu kwa nguvu ya jina lake tu. Hakutazamia vilevile kwamba pahali pa malazi yake ya mwisho patazuriwa mara kwa mara kama ilivyo sasa.

Mimi, binafsi yangu, nilifika kaburini kwake wakati wa kuandika hadithi hii. Nitakuwa tayari kuizuru tena kwa maua yote mazuri niwezayo kuyafikia kila nijaliwapo nafasi ya kufanya hivyo.

Katika wimbo mmnoja mdogo, lakini usiosahaulika, mwanamke

huyu alisema:

Siri sifunue

wino wa rangi,

Fahamu ujue

Kuna mambo mengi,

Wajila mwenyewe

Kwa ujinga mwingi.

Tazama kweli kubwa ilivyoelezwa kwa mistari myepesi na inayokumbukika! Kwa maneno machache na ya waziwazi aliweza kifingirisha kipopo cha fikira kubwa. Siti alikuwa mwenge wa kumulika johari katika pembe za giza za moyo wa mwanadamu.

Kama aliweza kuja tena katika dunia hii, sijui angalionaje kuwa kuona wasifu wake umefunuliwa kwa karatasi nyeupe na wino mweusi katika kitabu hiki!

SAFARI NA KUENEA KWA SAUTI YAKE

TARABU katika Kisiwa cha Unguja zilipokuwa zimeshughulika na Siti, viwanda vya santuri ugenini vilikuwa vimeshughulika na maongezo ya sahani za santuri katika dunia. Mashindano makubwa ya biashara hii yalitokea kati ya makampani. Kila tajiri alikuja katika uwanja na zabuni kubwa. Kampani ya Santuri ya Kolombia iliweka mfuko wake wazi kwa waimbaji na watribu wapya wa kila taifa. Ilipekua kaskazini, mashariki, kusini na magharibi. Ilipapasa Ulaya, Amerika, Asia, Australia na Afrika. Kila pembe ya ardhi ilimulikwa kwa uangaliful kutafuta watu kama hawa. Ilikuwa kama mwito wa taifa kuu kwa raia wake wajiunge katika majeshi. Wakati wa shani kubwa ulikuwa unapambazuka ghafula mbele ya dunia. Ilikuwa katika mwaka wa 1927.

Watu waliotakiwa walikuwa wastadi. Mtu kama mimi alikuwa hatakiwi. Fikiri kampani ya Santuri ya Kolombia ilichagua mtu gani katika Afrika Mashariki?

Mtu aliyechaguliwa alikuwa Siti. Alikuwa maskini wa sura lakini tajiri wa sauti. Heri kubwa ilianguka juu ya paja lake. Alipata mshahara mzuri. Melini alipewa chumba cha starehe na posho la kuchaguliwa, kama kwamba alikuwa mtoto wa watu kati ya abiria waliokuwamo.

Uchaguzi wa mtu wa kufaa kwa kazi maalumu uliongozwa na uwezo maalumu. Ilikuwa si kazi rahisi. Ilikuwa kazi ngumu kama kuchomoa ree katika jozi ya karata.

Mwanamume au mwanamke yeyote mwingine mzuri alikuwa hastahili uchaguzi ule. Palitakiwa sauti nzuri na uwezo wa kuimba, sio sura nzuri na urembo wa pambo. Mapendeleo yalikuwa hayana nafasi palipotakiwa ustahili mkubwa.

Katika Mei 1928 Siti moyo wake ulikuwa na kiu ya nchi ngeni, ambaye nyayo zake zilikuwa na mwasho wa safari, na ambaye hakutosheka na mwendo wa Fumba kijijini mpaka Unguja mjini katika wakati ule wote, alipata nafasi sasa ya kukanyaga kwa miguu yake vumbi la Bara Hindi. Alirudi Unguja akakaa kwa muda wa mwaka mmoja. Katika mwaka wa 1930 alikuwa tena katika safari hii.

Wenziwe katika safari ya kwanza walikuwa watribu watatu, nao walikuwa wanaume. Buda Swedi, Mwalimu Shaaban na Subeti Ambari. Watu wote wanne walikuwa wa Unguja. Unguja ilikuwa kama ghala ya waimbaji ya Afrika Mashariki katika wakati wa Siti. Katika safari yake ya pili alifuatana na Buda Swedi na Mwalimu Shaaban. Kufika kwao Bombay, waliungana na mtribu mmoja wa Misri aliyeitwa Muhidin Said, wakafanya kazi pamoja. Siti hakuweza kuimba kati ya watribu alizoea tu, lakini aliweza vile vile kutenda kazi yake hata kati ya mchanganyiko wowote wa watribu.

Wakati mmoja Siti alipokuwa akiimba mbele ya mtambo wa sauti kule Bombay, mmoja katika wenziwe alishikwa na majadi kwa sauti yake tamu akatamka ghafla: “Polepole, tuko mbali!”

Bila shaka walikuwa maili nyingi sana mbali. Lakini, maneno haya matatu madogo yaliota mbawa yakavuka bahari pana mpaka Afrika Mashariki. Si mtu huyu peke yake, hata watu wa Bara Hindi waliopata kusikia sauti ya Siti wakati ule, walishikwa na jazida ambayo nyepesi kufikirika, lakini ngumu sana kuelezeka kwa maneno ya mwanadamu. Siti alikuwa na sauti ya kulevya kweli. Ililevya watu katika Afrika Mashariki na katika nchi ngeni. Ilipenya sikioni ikatekenya mwili wa kila mtu kwa ladha yake. Watu waliopata kumsikia akiimba, wakumbuka hata sasa jinsi mioyo yao ilivyoyeyuka kwa furaha. Kwa safari hizi mbili sauti ya Siti iliokolewa katika maangamizi. Laiti zisingalitokea katika maisha yake, angalipotea katika bonde la sahau badala ya kupanda juu ya mlima wa umashuhuri. Kwa hivi, alifanya fadhili kubwa kwa watoto na wajukuu wa nchi yake. Katika wakati ujao wataweza kusikia santuri zao sauti yake ya ajabu iliyosisimua baba na mama zao, na babu na nyanya zao katika Afrika Mashariki kwa muda wa miaka thelathini na tisa.

Katika marejeo yake toka Bara Hindi, Watu Unguja walijipanga msitari forodhani kumpokea kama kwamba alikuwa malkia. Umati mkubwa, wa wanaume na wanawake, ulionekana katika wasiwasi. Baadhi ya watu waliweza kupata nafasi ya kuamkiana naye. Wengine hawakuweza kumfikia kwa msongano uliotokea. Hawa walitosheka na tazamo la haraka waliloweza kumtupia kwa mbali. Alikuwa kipenzi cha Kisiwa cha Unguja. Mapenzi ya nchi yalikuwa kitu muhimu sana. Mtu aliyeweza kuyapata alikuwa na hazina kubwa katika mikono yake nilitaka kusema alikuwa na msaada katika milki yake. Mtu aliweza kupata fahari gani nyingine kubwa sana kuliko ya kuwa na ya nchi na watu wake?

Mwanamke huyu aliweza kupata fahari kama hii. Siri gani ilimsadia katika fanaka yake? Alipata fanaka hii kwa sababu alikuwa mmoja katika watu wema waliopata kuishi. Sauti yake ilikuwa nzuri kama moyo wake, na moyo wake ulikuwa mwema kama sauti yake. Vitu hivi viwili mbalimbali, lakini vya sifa moja, alivitumia kwa watu katika wakati mmoja. Kwa hali hii aliajabiwa karibu na mbali akapendwa na kila mtu. Watu wa wakati wake hawakuweza kujizuia kumpenda. Je, wewe ungaliweza kumchukia kama ungalionana naye katika safari zake? Nadhani usingaliweza kufanya hivyo.

Siti alikuwa hana nafasi sasa ya kuweka tako lake kitini. Alipata mwito baada ya mwito. Pwani ilipokuwa ikimwita, bara ilikuwa ikimpungia nguo. Alitakiwa Unguja na Pemba. Alikaribishwa Tanganyika. Alitakiwa Kenya. Aliitwa Uganda. Nchi zote za Afrika Mashariki zilimpigia kelele. Simu zilikuwa moto kwa makaribisho yake. Alizuru kila nchi katika hizi mara kwa mara. Alipita akiimba sauti yake tamu katika miji mikubwa mpaka katika vijiji vidogo kabisa.

Katika mzunguko huu mkubwa hakujali kama aliwekwa vizuri safarini au alikokwenda. Alikuwa mtu maridhia, hakutaradhia lililokuwa haliwezekani. Hakujali vilevile kama alikwenda kwa miguu, motokaa au gari la moshi, katika jahazi au meli. Aliruhusu watu kumchukua mahali popote katika wakati wowote. Kama watu wavumilivu walipata

kuishi katika dunia hii. Siti alikuwa mmoja wao.

Safari zake zilikuwa nyingi sana kuliko mapumziko yake yalivyokuwa. Alikuwa katika mzunguko wa mkufu wa viungo vya safari daima. Hakupata kukataa mwito kwa udhuru wa uchovu katika maisha yake yote. Alikuwa hajui uchovu ulikuwa nini. Neno hili halikupita katika midomo yake. Hapana shaka, alikuwa na afya nzuri sana, au sivyo asingaliweza kwenda safari zile mara kwa mara.

Maisha yalikuwa na ajabu siku zote. Yalikuwa konde la kupanda mbegu ndogo mbalimbali zilizozaa mavuno makubwa. Hata kama mtu alikuwa mnyonge kama nini, kama alitenda neno lolote la maana, neno lile liliishi milele katika dunia.

Siti hakuzuka ghafla katika uzushi wala katika hadithi ziitwazo ngano. Alikuwa mtu kama watu wengine. Mambo aliyotenda yalikuwa makubwa kwa upande wake, lakini yaliigika.

Fikiri kama na wewe umepata kutenda neno lolote la fadhili kwa watu wa nchi yako. Kama hujalifanya bado, lifanye sasa. Yamkini una marafiki. Wafurahishe kwa fadhili yoyote uwezayo kutenda. Haikosi una washindani. Wape sababu ya kukuajabia kwa unyofu ulio nao. Wakati haukuumbwa kwa sababu ya kungoja mtu, unakwenda mbio mfululizo. Kama hukuuwahi utapatwa na hasara kubwa. Itakuwa kama uliyekuja duniani maskini, uliyeishi gizani na uliyeondoka bila kuacha alama. Maisha kama hayo yalikuwa hayafai kwa mwanadamu, ambaye kwa asili yake alitazamiwa kutenda mambo mengi. Maisha yalikuwa matendo, sio usingizi.

Kama Siti alitazama sura yake mbaya akasema kwamba hakuweza kutenda neno. asingalitenda jema lolote. kama alitazama rangi yake nyeusi akasema kwamba alistahili kuwa katika sahau, asingalikumbukwa na mtu hata mmoja, kama alijipima, akajiona alikuwa duni, asingalitukuka hata kidogo, na kama hakujaribu kufumbua tambo ya Maisha, asingalipata jawabu lake milele. Jaribu la kuimba bila alama yoyote ya muziki lilimwongoza mwanamke huyu katika sifa iliyoshangaza mawazo ya watu. Jaribu hili lilikuwa si ajabu katika Afrika katika karne moja iliyopita, lakini ni ajabu ya kutosha katika miaka hii ya kusoma na kuandika.

Mtu yeyote aliyetenda tendo bora alikuwa bora, potelea mbali wazazi wake walikuwa kina nani, kabila gani au rangi gani.

TABIA NJEMA

TOKEA mwanzo wa kusimulia wasifu wa mwanamke huyu haiwezekani kusemwa kwamba tabia yake haijatajwa bado. Labda imetajwa katika mahali pengi katika kurasa hizi kwa maneno ya kuzagaa kama nyota juu ya mbingu, au kama mtiririko wa mito katika ardhi. Walakini, juu ya kutenda hivyo hukubalika pia kwamba yote yaliyopata kutokea mbele yalikuwa mtajo wa neno moja au mawili katika sura mbalimbali. Kwa maneno machache, hili lilikuwa kama tazamo la haraka juu ya baadhi ya matendo yake mema yaliyochanua katika sura za kitabu hiki kama maua ya mimea mbalimbali katika bustani moja. Kwa kweli, huu ulikuwa kama mguso ambao ulishinda jaribu la kuepukana nao katika hadithi hii. Mguso huu ulikuwa hautoshi kuhesabiwa kama maelezo kamili ya tabia. Tabia ilikuwa jambo muhimu sana. Jambo lenyewe lilifungamana na hali yote ya kitu, mnyama au mtu katika maisha yake, sio sehemu yake moja tu.

Kwa mfano, kama ulimwengu ulitaka, uliweza kumpaka rangi chui yeyote mkali akawa mweupe, mweusi, mwekundu au fua, samawati au zari, kahawia au urujuani, kijivu au hudhurungi, kimanjano au kijani, lakini uliweza kufuga chui huyo kama kondoo kwa mashaka makubwa na hatari nyingi. Bila shaka, chui kama huyo angalipendeza macho ya watazamaji katika bustani ya wanyama, lakini mioyo ya watazamaji haohao ingalikuwa haina imani kwa hofu ya mazoea juu ya mnyama huyo. Kubadili ngozi ya chui kwa rangi kulikuwa kazi bure. Kwa desturi, umbo la chui lilikuwa si baya, lakini kadiri lilivyokuwa zuri ndivyo lilivyoficha uovu. Chui hakugeuzika kondoo, alikuwa mnyama wa kutisha siku zote. Kondoo hakubadilika chui, alikuwa mnyama mpole daima. Utaratibu wa kubadilisha chui kuwa vingine haujapatikana bado katika dunia.

Mfano kadhalika, iliwezekana kupamba mtu kwa elimu akawa mtaalamu wa sifa iliyoweza kuenea katika dunia kama nuru ya jua, lakini kama mtu yule alikuwa hana tabia ya kuvumilika, sifa yake ya elimu kubwa ilikuwa haina thamani. Alikuwa shetani mwovu katika umbo la mwanadamu.

Tabia ilikuwa mazoea nayo ilifanana sana na akili. Akili ilipotoka kwa fikira mbaya kama tabia ilivyoharibika kwa mazoea maovu, ilitengenea kwa fikira nzuri kama tabia ilivyokuwa kwa mazoea mema. Tabia ilitawaliwa na mazoea kama akili ilivyoongozwa na fikira. Aidha, kwa tabia ya kistaarabu, ambayo ilikuwa matokeo ya mazoea mema, mtu alikuwa bora kuliko mnyama, alikuwa juu ya viumbe wengine, na kwa tabia ya kishenzi, ambayo ilikuwa mazao ya mazoea mabaya, alikuwa dhaifu sana kuliko mnyama wa porini, alikuwa chini ya viumbe wote.

Kwa hali iwayo yote, katika umaskini au utajiri, ujinga au elimu, enzi au uraia, tabia ilikuwa kitu cha namna ya peke yake katika dunia, tena maongozi yake juu ya mtu yalikuwa tama. Tabia ilikuwa kama njia panda kuu katika maisha iliyogawa watu kwenda pande mbalimbali za dunia. Ilikuwa ufunuo wa ajabu wa nafsi ya mtu aliyepambwa na utajiri au aliyechafuliwa na umaskini, aliyependelewa na nguvu au aliyedunishwa na unyonge. Ilikuwa muhuri wa asili juu ya mtu wa adabu au aibu, hisani au nuksani, adili au ukorofi, uhiana au fadhili. Ilionyesha ukamilifu au upungufu wa mtu katika wakati wowote. Wema au uovu, manukato au uvundo, ulaini au ugumu, usafi au uchafu, huba au chuki, urafiki au uadui viliweza kuonekana katika nafsi ya mtu kama uso na kioo kwa tabia. Ilikuwa nuru katika giza la

nafsi ya mwanadamu. Watu walijulikana kwa tabia zao kama miti ilivyojulikana kwa matunda yake.

Tabia, kitu Cha mauzauza, ilikuwa pandio au mbawa kubwa kwa mtu. Iliweza kupeleka mtu wa kila namna katika urafiki mkubwa na majlisi mbalimbali kama ilikuwa ya adabu au amani, upole au Saburi, uaminifu au uungwana wa kutosha. Ilikuwa zuio au pingamizi kubwa kwa mtu wa aina yoyote katika urafiki na majlisi kama ilikuwa ya jeuri au kiburi, udanganyifu au ugomvi, ushenzi au utovu wa adabu. Heshima yoyote iliyokosa tabia njema ilikuwa kama taa iliyowaka juu ya nuru kubwa ya jua. Ilikuwa haina maana. Shina la ubaguzi na usawa wa watu ilikuwa tabia zao. Kama ilikuwa hivi, basi tabia ya mwanamke huyu ilistahili jaribu la maelezo chini ya sura mbali, au nyingine.

Kwa bahati mbaya, tabia ya wanawake ililaumiwa katika

pande nyingi sana za dunia kama kwamba wao walikuwa watenda maovu yote katika maisha. Pengine, hata ulevi, mama wa maovu, ulisifiwa wakati mwanamke alipolaumiwa. Acha mbali ulevi, hata kitu chochote kingine kilikuwa hakiwezi kulingana na mwanamke. Kwa kweli wanawake wa nchi yoyote hawakuonekana katika neno ambalo wanaume walikuwa hawamo. Kama mwanamke yeyote katika dunia alikuwa na tabia ya lawama, jambo ambalo lilikuwa jepesi kuweza, lakini gumu sana kuthibitishwa, tabia ya mwanamume yeyote ilikuwa si bora. Na mara lawama la jumla juu ya wanawake lingaliachiliwa mbali ingalikuwa vema kwa pande zote mbili.

Siti alikuwa na tabia ya kuajabiwa ingawa alikuwa mwanamke. Kama wanawake wengine walikuwa na umaskini wa johari hii, yeye alikuwa na utajiri wake. Alikuwa katika nuru ya tabia wakati baadhi ya wanaume na wanawake katika giza lake. Kwa miliki kama hii alionekana na amani na upole, saburi na unyenyekevu, uungwana na uaminifu kwa watu wa kila rika na wa hali mbalimbali. Alikuwa kipenzi kikubwa. Katika maisha yake mwanamke huyu alikuwa katika mwenendo wa tabia. Kama tabia yake ilihesabiwa kama gari ingalisemwa kwamba gari lenyewe lilitengenezwa vizuri sana. Lilikuwa na kiunzi cha saburi, mtambo wa bidii, magurudumu ya nguvu, sukani ya adili na siwa ya ucheshi. Katika gari hili la tabia, Siti alivuta hawa na mapendeleo ya watu toka kila upande kwa kipawa chake kikubwa cha sauti.

Kama Siti alikuwa hana tabia ya namna hiyo tegemeo lake lingalikuwa dogo sana katika maisha aliyoishi. Haijulikani angaliwezaie kujiokoa katika hatia isiyosameheka alipokuwa katika hasira na uchungu wa matusi! Hapana shaka, kwa matukano yale yaliyorarua kama kucha za chuma katika moyo wake, alikuwa katika maudhi yasiyoelezeka kwa lugha ya kitabu, lakini alivumilia. Alijua kwamba ilimpasa kupigana na wivu, masingizio, kashifa, ujinga na ulimwengu mzima kiungwana kama alitaka kufanikiwa. Alikuwa mwanamke mmoja katika wanawake waliokuwa imara kabisa.

Siti alikuwa mwanamke wa tabia kubwa ambayo hapana kitabu kwa Kiswahili kilichofundisha habari zake. Kama aliipata kwao nyumbani au katika unyago inatatiza kuhakikisha kwa sababu wasimulizi wake wote wamenyamaza kimya juu ya jambo hili. Siti hakujua wajibu wa tabia, kisha akaacha kutimiza kazi zake. Hakutumia tabia kama kisingizio au josho

baada ya kujichafua kwa tamaa za aibu. Alikuwa na imani nayo siku zote. Hakusema uongo, hakujilegeza, hakujipendekeza wala hakujifanya mtumwa. Alifanya kazi kwa bidii kila siku akajipatia ustawi kwa matendo yake mwenyewe. Bila shaka, alichukua miaka mingi kufikia ustawi wake, lakini hakushindwa. Na kila usiku aliweza kulaza kwa amani kichwa chake, juu ya mto, bila kusumbuliwa na mawazo mabaya. Lipi lililoweza kuwa bora kwa mwanamume au mwanamke kuliko kutazama nyuma ya maisha yake, akaona yalikuwa safi kama yungiyungi? Siti na tabia yake walikuwa kama marafiki wawili waliafikiana kabisa katika maisha. Baadhi ya watu walitaka usawa na uhuru wa matendo katika maisha haya yaliyojaa majaribu. Haja hizi mbili zilikuwa kubwa kwa watu, nazo kama ziliwezekana kupatikana kesho, ulimwengu mzima ungalikuwa katika furaha ajabu. Walakini, kama watu walikosa tabia wasingaliona uzuri wala furaha katika maisha ya usawa na uhuru. Wangalijiona katika uovu wasiopenda na huzuni isiyovumilika siku zote. Majuto ya ujinga wa kutaka kitu cha halali, lakini kilichokuwa hakijaandaliwa bado kushikwa vizuri lazima yangalikuwapo. Hili huenda likaonekana kama dhihaka katika maandiko, lakini hivi ndivyo lilivyo kweli katika maisha. Wingi wa hakika za maisha ya mtu zilifuata na mambo yaliyoitwa dhihaka mchana na usiku. Haiyamkini, hata kwa kiapo kwamba mtu aliweza kuwa mkubwa, bora, mheshimiwa au mwenye furaha kama tabia yake ilikuwa ndogo na dhaifu.

Siti alikuwa si mwanamke mkubwa, kwa kadiri ya wanawake wakubwa walivyojipambanua wenyewe, lakini alisaidiwa sana na tabia yake katika maisha. Kwa tabia yake ya ajabu alishawishi kila mtu kumjali katika kila pahali alipopata kufika. Alikaribishwa katika nyumba kadha wa kadha za heshima kwa hisani zote zilizowezekana kutendewa mwungwana. Alikuwa kipenzi kwa tabia kama si kwa cheo au nafasi.

Wakati mmoja Siti alipata heshima ya kuwa mwimbaji kwa Sultani wa Unguia. Jambo hili lilikuwa pendeleo kubwa kwake. Karibisho katika nyumba kubwa kama ya Sultani lilikuwa sawa na tuzo ya nishani ya heshima kwa mwanamke huyu. Fikiri, watu wangapi walitamani heshima kama ile lakini hawakuipata. Ilikuwa bahati kubwa ya maisha yake yote. Tokeo lake katika hadhara tukufu kama ile kama mwimbaji lilimpa nafasi ya makaribisho katika hadhara nyingi nyingine. Ilikuwa furaha kubwa sasa kwa mwanamke huyu, kuona nyumba ya Sultani imemfungulia milango

yake mikubwa! Kukanyaga miguu yake humo, kupiga magoti mbele ya utukufu wa Unguja, mabwana na mabibi walipokuwa wametega masikio yao kusikiliza sauti yake ya ajabu, na kuamini kwamba aliweza kupata msaada na himaya kwa mmoja wa masultani wa Afrika Mashariki ilikuwa fahari kubwa sana kwake. Alikuwa katika upeo wa furaha ya maisha yake.

Mwanamke alikuwa kama mwanamume katika dunia. Alipaswa kuwa na mambo yote aliyopaswa kuyafikia na ambayo yalikuwa wajibu katika maisha. Lakini katika mambo hayo, tabia ilikuwa jambo muhimu kabisa kwake. Alitakiwa kuwa nayo kama mwanamume alivyotakiwa kuwa na ubora. Siti alikuwa na tabia ya kutosha. Alikuwa na nanga nzuri sana katika maisha yake.

KUJIKIMU KISTAHIKI

KUJIKIMU ni kujiruzuku. Kujiruzuku ni kujitegemea kwa chakula, nguo na masurufu mengine katika maisha.

Kwa desturi, palikuwa hapana mtu aliyekuwa na lazima yoyote juu yake ya kuwa bora au duni, mkumbukwa au msahauliwa, mashuhuri au vingine katika ulimwengu kama yeye mwenyewe hakutaka kuwa hivyo. Lakini kwa hali iwayo yote, kila mtu, dhaifu au mtukufu, maskini au tajiri, jamali au vingine, alikuwa na lazima ya kupata riziki katika muda wote wa maisha yake. Faradhi hii ilikuwa msiba wa milele kwa mwanadamu katika dunia. Kwa maneno mengine, kiungo cha kwanza cha mnyororo wa utumwa katika maisha kilifuliwa na kanuni hii. Ilikuwa sharti moja katika masharti makubwa kabisa juu ya mwanadamu pamoja na haja zake. Kila mtu alitafuta amani, lakini palikuwa hapana hata mtu mmoja aliyeweza kuipata katika maisha haya ya uchungu wa haraka. Kila mtu aliabudu uhuru, lakini ilikuwa vigumu kuona mtu huru hata mmoja katika ulimwengu huu wa fadhaa ya kutumikia mwili. Uzito wa sharti hii katika maisha ulikithiri juu ya mabega ya mtu. Na kama kwamba hili lilikuwa halitoshi, tamaa yake ilipingwa na pingamizi, furaha yake ilikatwa na huzuni, shibe yake ilinyemelewa na njaa, ujana wake ulifukuzwa na uzee, afya yake ilitishwa na ugonjwa, na uzazi wake ulikuwa windo la mauti. Aliishi katika maisha ya mapigo mazito toka pande zote kama chombo kilichokuwa katika bahari ya dhoruba kali. Ilitaka imani kubwa katika moyo wake kuwaza habari za amani na uhuru katika hali hii.

Nataka sana ningaliweza kutumia neno zuri badala ya msiba, neno la huzuni kuu, lakini nimeshindwa kupata neno jingine linaloweza kusadifu vema. Napenda sana ningaliweza kutangua utumwa, neno la chuki nyingi katika ustaarabu wa sasa kwa neno lililopendeza, lakini mradi wangu haukufaulu kwa njia hii vile vile. Mimi si mtu peke yangu niliyepatwa na bahati mbaya ya kushindwa kama hivi. Wanaume kadha wa kadha wameshindwa na silaha zao mikononi. Mimi sikuwa na silaha. Nilikuwa na karatasi, kalamu na wino tu. Kushindwa kwangu kulikuwa si ajabu kubwa. Nadhani mtu yeyote angalishindwa kama mimi katika jaribu la kueleza

kinaganaga kila hakika au kweli ya maisha kwa maneno ya haiba na mvuto tu, ingawa ulimwengu ulijaa maneno hayo, yaliyoweza kueleza waziwazi baadhi ya fikira bora. Palikuwa na wingi wa maneno mema katika lugha kwa ajili ya mambo tulivyopenda, na wingi wa maneno mabaya kwa ajili ya mambo tuliyochukia. Kwa hivi, hakika mbalimbali za maisha katika dunia zililazimisha matumizi ya maneno mbalimbali, haidhuru kama yalikuwa mazuri au mabaya, machungu au matamu, magumu au mepesi, makali au vingine. Kusudi la lugha lilikuwa kutimiza kazi yake vizuri. Kwa kusudi hili, palikuwa hapana lugha katika dunia iliyotii upanga wala mzinga wa mtu. Kama ilikuwa hivi, palikuwa hapana faida ya kubana utumishi wake bora, kwa sababu ya kutaka kupendeza dunia iliyoshinda kila bidii ya kuipendeza. Matumizi ya maneno haya mawili yaliongoza katika kweli ya wajibu wa mwanadamu katika maisha yake.

Ilikuwa lazima juu ya mtu kufanya kazi kwa ajili ya maisha yake. Utaratibu wa ulimwengu ulikuwa hivi siku zote. Adamu alikuwa katika msiba na utumwa wa kazi kwa ajili ya maisha yake. Hii ilikuwa kweli kama kusema mbili na mbili ilikuwa nne. Na kweli ilikuwa na maana, tena ndiyo iliyosadikiwa. Ilipendwa na msemaji kama ilivyopendwa na msikizi, Ilipendeza kuwa nayo, ilipendeza kuweka, tena ilipendeza kutumia wakati wote katika maisha yetu. Kweli aikufa kiu kwa kiangazi, haikughariki kwa masika, haikutetemeka kwa baridi, wala haikulegea kwa hari. Haikuchakazwa na urefu wowote wa wakati. Ilikuwa na nguvu ya aushi katika nyakati zote za mwaka. Ungalipenda nini: uongo ulioficha uso wake katika giza ukapumbaa katika nuru, au kweli iliyomulika katika giza ikazidi uzuri katika nuru?

Katika mambo yote ambayo Siti alipata kutenda, namna yake ya kujikimu katika maisha ilikuwa kabisa, na kwa sababu hii, Afrika Mashariki ilikuwa na sababu kubwa ya kuona fahari juu yake. Mwili wa mwanamke huyu ulikuwa wake mwenyewe, hakuuuza katika wakati wowote kwa thamani yoyote ya utajiri. Nafsi yake ilikuwa yake mwenyewe, hukuiuza kwa heshima yoyote. Roho yake ilikuwa yake mwenyewe, hakuiuza kwa anasa yoyote. Alikuwa mwanamke wa mazao ya adili kubwa, si mazao ya

upotevu, aibu wala ulegevu. Aliuza kazi zake kwa fedha, anasa na heshima. Kwa sababu ya heshima yake, ilikuwa afadhali kwake kufinyanga vyungu, kuimba katika tarabu, kucheza katika natiki, au kufukua ardhi kwa kucha za vidole vyake mwenyewe kwa sababu ya riziki kuliko kuvunja utukufu ule mkuu wa mwanamke. Alikuwa johari gani katika dunia!.

Siku moja, katika Oktoba 1936 Siti alizuru Pangani, mji mmoja katika miji ya Tanganyika. Aliimba huko akapata tuzo ya shilingi elfu moja na mia mbili kwa usiku mmoja. Kwa jumla kama hii, yaonekana kama kwamba alituzwa kama shilingi mia moja kwa kila saa moja usiku ule. Alikwenda zake siku ya pili, lakini kumbukurnbu ya usiku ule ingali hai katika mioyo ya watu wa Pangani kama kwamba alikuwa mmoia katika watu walioweka msingi wa mji ule wa kale, au mashujaa Abushiri na Jahazi, walioutetea mbele ya shambulio la Nyundo (Hauptmann Emil von Zelewski).

Kwa njia hii, mwanamke huyu aliweza kuokoa jina lake katika orodha chafu ya tuhuma, akalitia katika orodha safi ya heshima. Kama mwanamke huyu hakustahili nishani ya sifa, kwa mwendo huu uliojaa adili na juhudi katika maisha katika dunia hii iliyotatiza watu wa kila namna, mwanamke gani mwingine aliyeweza kustahili heshima kama ile? Bila shaka palikuwa na wanawake wachache sana walioweza kuidai.

Kama ulihesabu ubora wa mtu kwa utajiri alioweza kukusanya katika dunia kwa pesa moja baada ya pesa moja ungaliweza kuona kwamba kosa kubwa la Siti katika maisha yake lilikuwa moja. Hakushughulika katika wakati wowote kutazama mara mbili kila aliyotumia. Alikuwa na harija kubwa katika matumizi yake. Kama ulihesabu ubora wake kwa mambo mengine, ungaliweza

kuona kwamba harija yake ilifidiwa na furaha aliyokuwa nayo katika moyo wake daima. Mwanamke huyu alikuwa na furaha kama mdiria kwa kuweza kujikimu mwenyewe kiungwana katika maisha ya wingi wa mashaka na uchache wa uhuru.

Sijui Siti angaliwezaje kujiokoa katika matumizi yake makubwa! Alikuwa msafiri wa kuzuru huku na huko. Alikuwa mgeni wa watu wote katika Afrika Mashariki na mahali pengine. Wasafiri walijua sana kupokea wasafiri wenzao waliokutana nao safarini. Mioyo yao ilikuwa wazi kama

mikono yao. Hawakuweza kufumbata pesa walipodhani ililipa deni la fadhili. Siti alifadhiliwa sana katika mahali pengi. Ilikuwa maumbile ya mwanamke kulipa fadhili. Aliona afadhali kufa maskini kuliko kuvunja jina lake katika tamaa ya kukusanya utajiri uliokwenda katika mfuko.

Kama Siti, mwanamke ambaye kwa sababu zote hakupata nafasi ya kupata elimu aliweza kwenda mwendo mwema kama huu, fikiri wewe mwenyewe, mwanamke aliyeweza kupata nafasi ya kutosha ya kuelimisha angalikwenda mwendo gani? Bila shaka, angalikwenda mwendo bora mara mia au elfu kuliko huu. Angaliweza kuleta msaada bora katika maendeleo ya nyumba, nchi na taifa lake kwa njia mbalimbali. Kwa udhahiri kama huu, palikuwa na shaka kubwa kama malawama na madai ya wajinga kwamba mwanamke alikuwa duni yalikuwa na maana au kweli yoyote. Ilikuwa upuzi na uzuzu ulioshikiliwa kama hekima na wakinzani kwa sababu ya ukinzani wa hasara kubwa kwa wanadamu na maisha yao.

Swali muhimu lililopatikana katika maisha ya mwanamke huyu wa ajabu lilikuwa moja. Namna gani ya wanawake ilitakiwa katika nchi hizi? Swali lenyewe lilitaka fikira za madiwani na serikali zao, na nchi na watu wake.

Mwanamke alikuwa mshirika kwa mwanamume. Aliungana naye kwa vifungo elfu nyingi vya mwili, damu na mfupa. Alifanana naye kama matone mawili ya maji yalivyofanana. Alikuwa ua la moyo, furaha ya roho na bustani ya mapenzi yake. Mashaka ya mwanamke yalikata katika moyo wa mwanamume kama shoka ilivyokata katika shina na tawi la miti. Kama alitakiwa aweze kujikimu kwa heshima kama Siti alivyotenda, nchi hizi zilikuwa na lazima kubwa ya kufikiri sana malezi yaliyoweza kuhimiza maendeleo yao. Hii ilikuwa si fikira ya kushika kwa ulegevu. Ililazimu kuzingatiwa barabara kwa koleo za ubongo katika kichwa ili isiponyoke hata kama tulisukumwa chini na mashaka ya ulimwengu. Macho ya watu yalitota kwa machozi kwa kuona kamari ya mwili, maisha na roho ya mwanamke kwa ajili ya riziki iliyowezekana kupatikana kwa wingi kwa njia nyingine. Mwanamke alikuwa na haki ya kupata nafasi kama ile ya mwanamume katika maendeleo. Ustahili wake wa jambo hili ulikuwa mkubwa sana. Palikuwa hapana maana wala faida yoyote ya kutoa nafaka kwa mwanamume, na kumvi kwa mwanamke. Maisha yalikuwa kama dhamana kubwa kwa mwanamume kama yalivyokuwa kwa mwanamke.

Dhamana hii ya shirika ilipasa kutunzwa kwa uangalifu wa watu wote wawili, na kwa thamani yoyote iliyotakiwa katika dunia kwa sababu ilihusiana na mambo mengi ya taifa la mwanadamu.

Baadhi ya wazazi walitukuza mabinti zao kama kwamba walikuwa malaika. Ilikuwa vema sana. Walakini, walipofanya hivi hawakujali kuwafundisha neno lolote la kutenda juu ya kujikimu wenyewe katika nyakati za dhiki. Mabinti kama hao walikuwa hawawezi kusimama kwa miguu yao msaada wa wazazi wao ulipokosekana kwa mabadiliko ya

maisha. Maisha yalibadilika mara kwa mara kama kinyonga. Kama watu walipenda au hawakupenda mabadiliko yake, maumbile yalikuwa kiziwi juu ya kicheko au kilio chao. Maumbile yalifanya kazi yake bila kujali kama mtu alifurahi au alihuzunika. Kama maisha yalibadilika kwa wema ilikuwa heri kwa mtu. Ilikuwa vigumu kwa mwanamke aliyekuwa hawezi kujitegemea mwenyewe kama maisha yalibadilika vibaya kwake. Jambo bora lilikuwa kujaribu kuweka tayari kila mwanamke, katika utoto wake, kwa heri au shari na mabadiliko ya Maisha katika dunia.

Nchi ilitawaliwa na serikali kama mtoto alivyotawaliwa na mzazi. Palikuwa hapana serikali yoyote ya busara duniani kupeleka jeshi lake katika vita bila silaha. Ilipeleka jeshi lililopata taaluma ya vita na silaha njema. Jeshi kama hilo lilitazamiwa ushindi. Ajali yote ya nchi ilitegemea juu ya jeshi hilo. Mfano kadhalika, mzazi yeyote aliyekubali kutia mtoto wake - mwana au binti - katika mabadiliko makubwa ya maisha bila mwongozo wowote alichekesha kabisa. Nafasi za ustawi wa mtoto kama huyo katika dunia zilikuwa tano kwa mia moja. Alikuwa mtoto aliyetumbukizwa kwa ghafla katika bahari ya mawimbi makubwa ya matata ya maisha. Ajali yake ilikuwa kushindwa mara nyingi sana kuliko bahati yake ya kushinda ilivyokuwa katika wakati wowote.

Imesemwa mara kwa mara kwamba katika maisha mwanamke alikuwa na mapigano mengi kama mwanamume. Kama hili lilikuwa si mzaha wa kupitisha wakati, basi ilikuwa wajibu wa kila nchi kuandaa wanawake wake wote kwa mapigano yao. Kufaulu kwao kulikuwa kushindwa kwa watu wote. Umati wa wanawake wa kazi na matendo mbalimbali kama Siti alivyokuwa ndilo jeshi lililotakiwa katika wokovu wa maisha katika Afrika Mashariki. Kufurahia kashifa ya wanawake katika magazeti wakati baadhi

yao walipoweza kujipambanua kama wanaume ilikuwa upuzi mtupu. Kama palipatikana Siti mmoja aliweza kuimba, paliweza kupatikana Masiti wengine vilevile kwa kazi mbalimbali. Mabinti wangapi wema walizaliwa katika Afrika Mashariki kila siku? Mia za mabinti kama hao walioza kwa mafunzo mabaya.

Natamani ningaliweza kuthibitisha sifa peke yake kwa walimwengu juu ya adili ya Siti katika maisha yake, lakini kwa hali yoyote hilo lingalionekana neno geni sana katika wasifu huu. Katika dunia hapana mtu aliyeweza kuishi katika maisha ya adili bila lawama. Siti alikuwa mtu kama watu wengine. Hadithi yake imepasa kusimuliwa kama ile ya mtu yeyote aliyepata kuishi duniani. Kama adili yake imeonekana katika kujikimu kwake kwa heshima, lawama lake limetokea pia katika matumizi yake ya fedha. Kwa matumizi yake makubwa alikuwa maskini siku zote, lakini kwa adili yake ya ajabu ameacha kitu kingine nyuma yake. Ameacha johari ya jina lake kama urithi kwa watu wote wa wakati ujao. Isitoshe, amepiga siwa iliyokuwa inangojewa sana kuamsha bidii iliyolala katika mioyo ya wanawake juu ya wajibu wao wa kujikimu kiungwana katika maisha.

Kwa desturi dunia haichakai, ilichakaza vitu vilivyokuwa ndani yake. Kama machimbo ya kina yalifanywa katika ardhi, au minara mirefu ilijengwa juu yake, ilikuwa mamoja. Kanuni ya dunia ilikuwa kuchakaza watu pamoia na maisha yao, isipokuwa majina ya watu walioweza kujipambanua kwa matendo yao. Tendo kubwa kabisa ambalo mtu aliweza kutenda liliacha mchoro mdogo kabisa katika uso wa dunia. Alama hiyo ndogo ilikuwa ndiyo tofauti yote ambayo mtu aliweza kutenda katika maisha yake. Kwa hivi, kama iliaminiwa au haikuaminiwa, mtu aliishi tena katika dunia iliyomchakaza

kwa alama aliyoweza kuacha nyuma yake. Katika watu walioacha alama kama hizo, Siti alikuwa mmoja wao. Itakumbukwa kwamba katika kijiji cha kwao, mwanamke huyu alijulikana na watu wa kijijini, katika mji wa Unguja alikuwa si maarufu sana kuliko mwanamke yeyote wa mjini, lakini baadaye kwa jina aliloacha nyuma yake, amekuwa fahari ya Afrika Mashariki na dunia nzima. Ameacha kitu bora kuliko kimeta cha nuru katika giza la maisha na kujikimu.

ORODHA YA MANENO NA MAANA ZAKE

manzili - maelekeo, upeo.

yametoweka - yamepotea kama mvuke.

Ilipozinduka - ilipotoka usingizini, ilipoamka.

mashuhuri - enye sifa kubwa.

Wazalia - waliozaliwa.

umbu - dada, ndugu mwanamke kwa baba au kwa mama.

Shajara - hapa maana yake desturi.

fauka - sembuse, licha.

Fahari - utukufu, ukuu.

maumbile - mahuluku, tabia.

umaarufu - utukufu.

Kadhalika - pia.

watabiri - wabashiri.

usahihi - kuwa sawa bila makosa.

usichana - kuwa kijana mwanamke.

yamkini - huenda ikawa.

Maskani - mahali pa kuishi.

Mahari - malipo ya ndoa.

Utosi - katikati ya kichwa.

Magae - vipande vya kitu kilichovunjika.

Kazi ya kijungu jiko tu - kazi ya kujipatia chakula tu.

Akajitanda - akavaa kufunika mabega.

Vichochoro - njia nyembamba.

Alinadi - alitangaza.

Wakambeza - wakampuuza.

Kutumbuiza - kufurahisha (kutumbuiza, kufurahisha, kustarehesha).

Hawa ya Maisha - furaha ya Maisha.

Sudusu - sehemu moja katika sita.

Shauku - mapenzi, tamaa.

Ilivokabili - sogelea, kuwa mbele ya aghalabu kwa kawaida.

Nadra - mara chache, haba.

Sarafu - kipande cha fedha, matumizi.

Ushawishi - kushawishika, kuvutia kwa tamaa.

Walikuwa kama shilingi - walifanana kabisa.

Mila - tabia ya asili.

Ujasiri - uhodari wa kufanya jambo bila hofu.

Kuhidiwa - kugeuza ili ifae, ongowa.

Kutanguliwa kuvunja, - kuondoa, kuachilia mbali.

Ratibu - kupanga mambo kwa utaratibu.

Fanaka - kufanikiwa.

Alipumua - alipumzika.

Sulu - dawa ya kusafisha(asili yake ni kizulu sula safisha).

Kukwatua - kutakasa.

Udi - kinanda cha nyuzi kama gambusia.

Mahiri - hodari, stadi.

Kipawa - uwezo, kipaji.

Tamasha - furaha.

Mwanagenzi - mwanafunzi, mtu afundishwaye kazi.

Ghasiafujo - rabsha.

Ilidumisha - iliendesha siku zote.

Ari - moyo wa kupenda kutimiza jambo.

Kinyumenyumena kimbelembele - mbele na nyuma (kujua vizuri sana).

Nahau - sheria na matumizi ya lugha safi.

Kuhifadhi - kuweka vizuri isiharibike.

Kuyakariri - kujifunza kimoyomoyo, kurudia rudia.

Jumuia - chama, umoja.

Watribu - waimbaji, waghani.

Maarufu - wanaojulikana sana.

Gambusia - kinanda cha nyuzi.

Majiya nazi yaliyokuwa yakingoja mvungilo - maji ya nazi yalikuwa yanangoja njia ifunguliwe ili yapate kutoka na kumwagika.

Maridhawa - tele, ya kutosha kabisa.

Fidla - kinanda cha uzi.

Ala - chombo cha kufanyia kazi.

Tarabu - furaha ya ngoma ya vinanda.

Ilimkabili - ilimsogelea, ilimfika.

Kikwamo - kikwazo, tatizo.

Mwunzi - mruzi, kupiga filimbi kwa mdomo.

Dhamira - nia.

Kusulubika - kupata taabu, kuteseka, kufa msalabani.

Akazuka - akatokea ghafla.

Madaftari - vitabu vya hesabu.

Pingamizi - kizuwizi, mgogoro.

Dhiki - shida.

Johari - jiwe la thamani, kito.

Chaza - namna ya Samaki wa maji chumvi, simbi.

Kimelea - kiduha, mmea unaoharibu mimea mingine kwa kuinyan'ganya chakula.

Madaha - namna, mtindo.

Kiada - kikawaida, kisheria, kidesturi.

Rika - kila makamo.

Shauku - tamaa, uchu.

Uliokithiri - uliozidi kiasi.

Tarabu - mchezo wa vinanda, tamasha.

Vipawa - uwezo.

Natiki - mchezo, namna ya ngoma, manyago.

Yamkini - yawezekana.

Hadhara - mbele ya umati wa watu.

Majadi - sehemu za mchezo, juhudi, asili.

Halipepesi - halitembei, halifumbi na kufumbua.

Kutuzi - harufu mbaya, kikwapa.

Fulfa - vibaya, namna isiyopendeza, hovyo.

Mzaha - utani, mchezo.

Afriti - shetani, pepo mbaya.

Adili - juhudi, bidi.

Tafrija - furaha kubwa.

Hiana - ubaya, moyo usiopenda mwingine apate.

Kuvisuluhisha - kuvipatanisha, kuviwezesha.

Ukinzani - upinzani, kubishana.

Faraja - poza moyo, kitulizo.

Adimu - inayopatikana kwa shida.

Karimu - mtu mwema, mtu anayetoa bila kuombwa.

Mkataba - mapatano.

Neema - tunuku, zawadi ya rehema.

Kubatilisha - kuharibu.

Kadha wa - kadha jumla, vivi hivi.

Ghairi ya - licha ya, isipokuwa.

Utanashati - utamaduni, ustaarabu, malezi mazuri, urembo.

Umahiri - ustadi, ufundi.

Mlahaka - ujuzi wa kuamkiana (laki kuta, onana, pokea).

Lilishwawishi - vutia, jaribu.

Duni - dhaifu, nyonge, si kitu.

Nasaba - asili, ukoo, jadi.

Husuda - wivu, jisho baya.

Ngoa - ngera, wivu.

Karaha - chuki, kasiri, jambo linalochukiza.

Nazaa - kashifa, aibu, simbule.

Kashifa - aibu.

Ulidara - uliwashika (watu), uliwavuta, uliwaathiri.

Mawe! - Sivyo! Hapana!

Dhila - hali ya chini, hali mbaya.

Waivu - waliomwonea wivu, wenye wivu.

Muhimu upesi, haraka, mbio.

Si mtoto wa watu - si mtoto wa ukoo mtukufu.

Jamali (jamili) - ya kupendeza, nzuri.

Si kifani chake - si kitu cha kulinganisha naye.

Ajabu akidi - ajabu kubwa, siti bibi.

Aula - afadhali, hiki ni aula kuliko.

Yalimhini - yalimnyima.

Mawe! - Sivyo! Hapana!

Dhila - hali ya chini, hali mbaya.

Waivu - waliomwonea wivu, wenye wivu.

Muhimu - upesi, haraka, mbio.

Kuhidiwa - kuongolewa, kutoka katika mwenendo mbaya

Azizi - tunu, ajabu, thamani, bora.

Utawa. - kukaa ndani na kufuata sheria ya kutotembea ovyo, kuwa ndani kama mwali, hali ya kuishi Maisha mema.

Aushi. - kudumu.

Bure ghali - haifai hata kupewa bure.

Uliviza - ulizuwia mawazo.

Mradi - haja, makusudio, nia.

Rasi - utosi, katikati ya kichwa, nchi iliyochomoza baharini, juu ya (kitu).

Maridhawa - tele, yakutosha, mengi.

Nakawa - yakuteua, nzuri, bora.

Libasi - pambo la mwili, kivazi.

Teule - iliyoteuliwa au kuchazuliwa.

Tunu - hamu.

Holi - mwenendo, chombo cha kulishia Wanyama.

Mbadhilifu - anayetumia kwa fujo.

Kilichomfaulisha - kilichomfanya afaulu.

Wimbi la jaha - wimbi la neema, kufaulu.

Kufumba na kufumbua - punde si punde.

Mauko - kifo, kufa, tendo la kuondoa.

Kashifa - sifa mbaya.

Usiri - kuchelewa chelewa.

Jadi kubeli - jedi bora, asili kubwa.

Latifu - nzuri.

Nyuso zao zilishuka kwa aibu. - waliona haya.

Nazaa - aibu.

Purukushani. - kujitia hamnazo, kujifanya huoni kumbe unaona.

Kuudondoa - kuufuata neno kwa neno.

Watani - uzawa, heshima ya kuwa mzalendo.

Kusadifu - kufaa, kuwa barabara.

Ibra - ajabu.

Hakufadhaika - kuhofu, kushangaza, kupambaa.

Mteuzi - mchaguzi.

Adimu - isiyopatikana kwa urahisi.

Shani kubwa - ajabu kubwa.

Tua - ajali (z)aibu, Upuugufu.

Kusawiri - kuandika picha.

Sitawa sitawi - kuwa na hali njema.

Ujamilifu - kukusanyika, ukamilifu, kufanya kuwa kizuri.

Hedaya - zawadi.

Michomo - kinachochoma moyo.

Kinywa cha salata - maneno ya waongo ya uzushi.

Utumbuizo - kufurahisha kwa sauti tamu.

Haikuhinikizwa - haikufunikwa au kuzuiliwa.

Hadhaa - mahali palipohudhuria watu.

Mtu wa mrua mkubwa - mtu wa heshima.

Bingwa - fundi mkubwa, mshinde.

Akajiandaa - akajitayarisha.

Kukughairi - hakuchukia, au kuegiza nia yake.

Kashifa - sifa mbaya.

Wakamwandama na kofia mikononi. - Wakamfuata kwa heshima na pupa.

Aliajabiwa - alionewa ajabu, alishangaliwa.

Majilio yake - kuja kwake.

Ari - moyo wa kupenda kitu.

Turufu - ni karata yenye nguvu.

Kipupwe - wakati wa baridi kali.

Wateule - watu wenye heshima, walioteuliwa.

Alaghani - aliimba vizuri.

Mbubujiko - kutiririka kwa maji.

Uta - upinde.

Fani - elimu, ujuzi.

Ladha - utamu.

Ushiridu - wimbo, utungo, ushairi.

Duka laku adhima - Dua la mola mtukufu.

Mwadhama - mtukufu.

Moya hayu el kaima - Mungu alie hai daima.

Astahaki salama - anastahili kuwa salama.

Jibli - kizazi, asili.

Janati - bustani, pepo.

Naima - bora.

Jalali - tukufu.

Muhtarima - mchaguliwa, mteuliwa.

Maulana - bwana, mtukufu, mola.

El Fadhili - mpaji, mtendea mema.

Atabduu - afike, aje.

Shamshama - aliyewekwa katika nuru, au mwenyenguvu (Sultan).

Astahaki - astahili.

Salama - amani, uzima, wokovu.

El amiri - mwenye amri juu yaw engine.

Tamati - mwisho, kikomo.

Nadhama - utungo, shairi.

Ghulama - Watoto.

Tamko - neno, usemi.

Hakuajabiwa - hakuonewa ajabu, hakuonekana ni waajabu.

Alifululiza - aliendelea bila kusimama.

Korija - vitu ishirini kwa pamoja.

Tarabu - ngoma ya vinanda kama gambusia.

Watribu - waimbaji katika taarabu.

Chonjo - ushawishi, fitina.

Rai, - taratibu kubembeleza.

Hakuhini - hakunyima, au kufanyia wivu.

Nyenzo - uwezo, nguvu.

Sahala - wepesi.

Takilifu - bila kupenda.

Umashuhuri - utukufu, ubora.

Mauko, kifo - maanguko.

Patazuriwa - patatembelewa (zuru v. kagua).

Wajila - wa (wewe) jila (kula) m.y. unakula mwili wako wewe mwenyewe.

Kufigirisha - kusukuma kama gurudumu.

Kipopo - kinyama kidogo kama panya kirukacho kwa mbawa,kipigio k.m. kipopo cha kuangulia embe.

Zabuni - tia filisi mnadani, taka kununua.

Ree - aina ya karata yenye alama â€˜Aâ€™ (Ace).

Majadi - hali ya kupenda sana, shauku.

Jaziba - kushikwa na shauku.

Ladha - utamu (onja, harufu).

Fadhili - tendea wema, wema (n.).

Fanaka - mafanikio.

Aliajibiwa - alionewa ajabu.

Yeye na wake jibli - yeye na kizazi chake.

Wende janati naima - wende katika Bustani ya peponi.

Abdallah jalii - mtukufu

Abdallah (mwanaye Sultani). - Said muhtrima Said (jina) mteuliwa.

Maulana el Fadhili - Bwana atendaye mema.

Atabdui shamshama - afike aliyewekwa katika nuru.

Astahiki salama - astahili (ana haki ya) salam.

Maulana el amiri - Bwana mwenye amri juu yaw engine.

Tamati nahitimisha - mwisho namaliza.

Ndiyo mwisho wa nadhama - ndiyo mwisho wa utungo (shairi.)

Rabi akupe Maisha - Mungu akupe Maisha.

Wewe na wako ghalama - wewe pamoja na Watoto wako.

Hapa bahati imekwisha - hapa shairi limekwisha.

Nahofu wako kalima - nahofu neno lako, (usemi wako).

Astahaki salama - astahili salama.

Maulana el amiri - Bwana mwenye amri juu yaw engine.

BWANA MTAWALA.

Bwana (Said) bin Harub

Ndiwe mhisani wetu

Mungu akupe uwezo

Ashindwe adui yako

Upate unachokitaka

Ishi milele

Anastahili kuwa salama

Bwana Mtawala.

Mungu atakuepusha na baya

Unusurike kiongoz

Pasiwe rntu wa kukudhuru

Mpaka mwisho wa Dunia

Ufanye kazi yako ya kuamuru

na kufunga

Wabaya wasiofuata sheria

Anastahili kuwa salama

Bwana Mtawala.

Bwana ulipoondoka

Raia tulihuzunika

Sote tulikuwa wanyonge

Tukaonyesha ukiwa

Na sasa umerejea

Tutaanza kunenepa

Anastahili kuwa Salama.

Bwana Mtawala

Mungu atakuweka

Kiweko kilichotimia

Utakalo utapata

Ili hali adui anaona

Kwa kila jerna upewe

Nguvu na amani

Anastahili kuwa salama

Bwana Mtawala.

Bwana Mola mzidishie cheo

Makamu yake yazidi

Umwondolee na maradhi

Awe mzima milele

Kwa baraka za Ibadhi

Nguvu zake Mola

Anastahili kuwa salama

Bwana Mtawala.

Yeye na ampendae

Waingie peponi

Abdallah kipenzi

Mheshimiwa Said

Bwana Mkarimu

Amshinde adui

Anastahili kuwa salama

Bwana Mtawala.

Mwisho namaliza

Ndiyo mwisho wa nia

Mungu akupe maisha

Wewe na wapenzi wako

Hapa zimekwisha

Nahofu ewe Bwana

Anastahili kuwa salama.